JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2021

## UALIMU

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2021

# 610 UALIMU

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ..... iv
1.0 UTANGULIZI ..... 1
2.0 TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI ..... 2
2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi ..... 2
2.1.1 Swali la 1: Saikolojia ..... 2
2.1.2 Swali la 2: Mtaala ..... 5
2.1.3 Swali la 3: Tathmini katika Elimu ..... 7
2.1.4 Swali la 4: Nadharia za kujifunza ..... 10
2.1.5 Swali la 5: Saikolojia ..... 13
2.1.6 Swali la 6: Elimu ya watu wazima ..... 15
2.1.7 Swali la 7: Ufundishaji ..... 18
2.1.8 Swali la 8: Upimaji katika Elimu ..... 20
2.1.9 Swali la 9: Uongozi wa Elimu Tanzania ..... 22
2.1.10 Swali la 10: Matayarisho ya Ufundishaji ..... 25
2.2 SEHEMU B: Saikolojia ya Elimu ..... 28
2.2.1 Swali la 11: Saikolojia ..... 28
2.2.2 Swali la 12: Makuzi na Ukuaji wa Mtoto ..... 34
2.3 SEHEMU C: MITAALA NA UFUNDISHAJI ..... 40
2.3.1 Swali la 13: Ufundishaji ..... 40
2.3.2 Swali la 14: Ufundishaji ..... 46
2.4 SEHEMU D: UTAFITI WA KIELIMU, UPIMAJI NA TATHMINI ..... 52
2.4.1 Swali la 15: Tathmini katika Elimu ..... 52
2.4.2 Swali la 16: Utafiti katika Elimu ..... 56
2.5 SEHEMU E; MISINGI YA ELIMU ..... 60
2.5.1 Swali la 17: Maendeleo ya Elimu Tanzania ..... 61
2.5.2 Swali la 18: Elimu Jumuishi ..... 65
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA ..... 72
4.0 HITIMISHO ..... 73
5.0 MAPENDEKEZO ..... 73
Kiambatisho ..... 74

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa taarifa ya uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika somo la Ualimu kwa wahitimu wa Daraja la A mwaka 2021. Taarifa hii imeandaliwa kutoa mrejesho wa ufaulu kwa wanachuo, wakufunzi, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla.

Mtihani huu ni tathmini ya mwisho ambayo pamoja na mambo mengine, inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Ualimu. Kimsingi majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa kipi mfumo wa elimu umeweza au umeshindwa kuwapa watahiniwa walipokuwa katika mafunzo ya Ualimu katika Daraja hili.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vizuri, wastani au vibaya katika mtihani huu. Watahiniwa walio wengi walifanya vizuri katika mtihani wa somo la Ualimu. Watahiniwa hawa waliweza kutambua mahitaji ya swali, walionekana kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada husika, walielewa vizuri dhana mbalimbali zilizotahiniwa, walikuwa na uwezo wa kujibu maswali kulingna na nyanja husika na walikuwa na maarifa ya kutosha katika uandishi wa insha. Aidha, wachache walishindwa kufanya vizuri, kwa kuwa walishindwa kufikia vigezo vilivyoainishwa.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika maswali waliyojibu unatoa picha halisi ya mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Ualimu katika vyuo vya Ualimu Tanzania.

Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, wakuu wa vyuo, wakufunzi na wanachuo kutumia mbinu muafaka ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Maboresho hayo yatasaidia kuinua kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika mitihani ijayo inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Mwisho, Baraza linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, Wakufunzi na wadau wote waliohusika katika uchambuzi wa takwimu na kuandaa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Ualimu kwa Watahiniwa wa Ualimu ngazi ya Astashahada ulifanyika mwezi Mei, 2021 na uliandaliwa kwa kuzingatia Muhtasari wa somo la Ualimu wa mwaka 2009 Ngazi ya Cheti Elimu ya Msingi.

Mtihani ulikuwa na maswali kumi na nane (18) na mtahiniwa alitakiwa kujibu jumla ya maswali kumi na nne (14) kutoka katika sehemu A, B, C, D na E. Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ya majibu mafupi ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote na kila swali lilikuwa na alama nne (04). Sehemu B, C, D na E zilikuwa na maswali mawili (02) ya insha kila moja, ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja kutoka kila sehemu. Kila swali katika sehemu B, C, D na E lilikuwa na alama 15.

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika somo la Ualimu kwa mwaka 2021 kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 2,946 (99.9%) waliofanya mtihani walikuwa na ufaulu wa wastani hadi mzuri. Aidha watahiniwa 4 tu (0.1%) kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walipata alama chini ya wastani.

Ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika viwango vitatu ambavyo ni ufaulu mzuri, wastani na hafifu. Ufaulu mzuri unaanzia alama 70 hadi 100, wastani alama 40 hadi 69 na hafifu alama 0 hadi 39. Aidha, kiwango cha ufaulu kwa kila swali katika sehemu A ni *kizuri* ikiwa watahiniwa watapata alama kati ya 3 na 4; kiwango cha *wastani* ni kati ya alama 2 na 2.5 na kiwango *hafifu* ni kati ya alama 0 na 1.5. Kwa maswali ya sehemu B, C, D na E, kiwango cha ufaulu katika kila swali ni *kizuri* ikiwa watahiniwa watapata alama kati ya 10.5 na 15; kiwango cha *wastani* ni kati ya alama 6 na 10 na kiwango *hafifu* ni kati ya alama 0 na 5.5.

Katika kufanya uchambuzi na kutafsiri ufaulu wa watahiniwa, chati za viwango vya ufaulu zimeambatishwa ili kufafanua ufaulu kwa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano ufaulu wa wastani na rangi nyekundu ufaulu hafifu.

Taarifa hii inachambua maswali yaliyojibiwa vizuri, wastani na hafifu. Uchambuzi huu unalenga kuonesha jinsi watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani wa somo la Ualimu. Sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatishwa ili kuonesha waliofanya vibaya na waliofanya vizuri. Aidha, taarifa inaonesha sababu zilizowafanya baadhi ya watahiniwa kupata au kutopata alama za juu katika majibu ya maswali kwa baadhi ya mada. Hivyo,

uchambuzi huu utasaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Ualimu kwa mada hizo ili kuongeza ufaulu wa watahiniwa katika mitihani yao.

## 2.0 TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

### 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10), yaliyolenga kupima maarifa waliyoyapata watahiniwa katika somo la Ualimu. Maswali hayo yalitoka katika mada kumi (10) ambazo ni*: Saikolojia, Mitaala, Tathmini katika elimu, Nadharia za kujifunza, Elimu ya watu wazima, Ufundishaji, Upimaji katika elimu, Uongozi wa elimu Tanzania, na Matayarisho ya ufundishaji*. Kila swali lilikuwa na alama nne (4) hivyo kufanya jumla ya alama arobaini (40). Katika sehemu hii ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu ambapo, mtahiniwa alikuwa na ufaulu hafifu endapo alipata alama kuanzia 0 hadi 1.5, ufaulu wa wastani alama 2 hadi 2.5 na ufaulu mzuri alama kuanzia 3 hadi 4.

#### 2.1.1 Swali la 1: Saikolojia

Swali liligawanyika katika vipengele (a) na (b) ambapo katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi maana ya Saikolojia na katika kipengele (b) kubainisha faida tatu za kusoma Saikolojia. Jumla ya watahiniwa 2,950 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 98.5 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 1.




***Chati Na. 1:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa watahiniwa (1.5%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5; watahiniwa (25.5%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa (73%) alama kuanzia 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi 2,154 (73%) waliopata alama kuanzia 3 hadi 4 walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Saikolojia* hususan kipengele cha *dhana ya saikolojia*. Watahiniwa hawa walielewa vema matakwa ya swali hivyo walitoa majibu sahihi. Mfano katika kipengele (a) waliweza kutoa jibu sahihi ambalo ni: *Saikolojia ni taaluma ya sayansi inayohusu mchakato wa akili, tabia na mwenendo wa binadamu.* Aidha, katika kipengele (b) waliweza kuainisha faida tatu za kusoma saikoloijia ambazo ni: *inasaidia katika kurekebisha tabia na mienendo isiyofaa katika jamii, inasaidia kubaini matatizo mbalimbali katika jamii na inasaidia kutatua changamoto na matatizo mbalimbali katika jamii.* Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya watahiniwa katika swali la 1.



1(a) Saikolojia- Ni tawi la kisayansi linalojishughulisha na tabia pamoja na mienendo ya binadamu pamoja na wanyama.
Saikolojia inaweza kuwa ya Elimu, viwanda, hospitalini na kilimo pia.

(b) Kutambua tabia na mienendo ya wanafunzi Shuleni.
- Kufundisha kwa kuzingatia umri na uelewa wa wanafunzi.
- Kutatua matatizo mbalimbali kabilka jamii kwa kutoa ushauri na unasihi.

Kielelezo Na. 1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 1

Aidha, watahiniwa 753 (25.5%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 kwa sababu walikuwa na dosari mbalimbali katika majibu yao hivyo walishindwa kupata alama zote nne. Wengi wa watahiniwa katika kundi hili walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na wengine walitoa majibu pungufu au maelezo dhaifu na hivyo walishindwa kupata alama za juu.

Watahiniwa 43 (1.5%) waliopata alama kuanzia 0 hadi 1.5 walikosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Saikolojia. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alitoa hoja zisizosahihi kama vile: *husaidia kujua maumbile na asili ya binadamu, husaidia kutupatia maarifa na ujuzi katika utendaji wa mambo mbalimbali na husaidia katika kufanya tafiti mbalimbali za kisayansi*. Mtahiniwa mwingine alieleza kuwa Saikolojia ni *sayansi inayojishughulisha na tendo la binadamu na wanyama katika maisha* na faida za kusoma Saikolijia ni kuwa: *inasaidia na kujua au kutambua vitu mbalimbali* ambapo mtahiniwa mwingine alitoa faida za kusoma saikolojia kuwa ni: *kupata stadi za maisha, husaidia kurahisisha utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii kwa kujenga hospitali na kutoa elimu juu ya masuala mbalimbali.* Kielelezo Na. 1. 2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kutoa majibu sahihi katika swali hili.



01. a) Saikolojia: Ni sayansi inayowezesha kujua ukweli wa wanafunzi katika nyanja kato wa ufundishaji na ujifunzaji.

(b). Faida za kusoma Saikolojia.

i) Husaidia kujua maendeleo ya mwanafunzi.

ii) Husaidia kujua changamoto za ufundishaji.

iii) Husaidia kujua mbinu mbalimbali za kufundishia na kujifunzia.

Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 1

Katika Kielelezo Na. 1.2 mtahiniwa alieleza maana ya Upimaji na faida za upimaji katika elimu badala ya kueleza maana ya Saikolojia na faida za kusoma Saikolojia.

### 2.1.2 Swali la 2: Mtaala

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuorodhesha sababu nne zinazoweza kuleta mabadiliko ya mtaala. Jumla ya watahiniwa 2,950 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 83% walipata alama kuanzia 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 2.




***Chati Na. 2:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa, watahiniwa (17%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5; watahiniwa (22.7%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa (60.3%) alama kuanzia 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 1,778 (60.3%) waliopata alama kuanzia 3 hadi 4 waliweza kuorodhesha sababu tatu hadi nne zinazoweza kuleta mabadiliko ya mtaala. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana nzima ya *Mtaala* hivyo walitoa majibu sahihi kama vile*; mabadiliko ya sayansi na teknolojia, tafiti mbalimbali zinazofanywa na wataalamu wa elimu, falsafa ya jamii na mahitaji ya jamii kuongezeka au kubadilika.* Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi.


2. (i) Mabadiliko ya sayansi na teknolojia
(ii) Tafiti mbalimbali zinazofanywa na wataalamu wa elimu.
(iii) Falsafa ya jamii
(iv) Mahitaji ya jamii kuongezeka au kubadilika.

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 2

Watahiniwa 671 (22.7%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5, ambapo baadhi yao walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na wengine waliorodhesha sababu pungufu au zisizojitosheleza hivyo walipata alama za wastani.

Watahiniwa 507 (17%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5 kwa sababu waliweza kutaja sababu moja tu ya mabadiliko ya mtaala. Watahiniwa 159 (5.4%) walipata alama 0 kwa sababu hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na sababu zinazopelekea mabadiliko ya mtaala. Baadhi ya majibu yasiyosahihi ya baadhi ya watahiniwa hawa ni: *kutofautiana kwa muhtasari, kukosekana kwa kitabu cha kiada, kukosekana kwa kiongozi cha mwalimu na kukosekana kwa kalenda ya masomo.* Mtahiniwa mwingine aliandika: *uboreshaji wa vifaa vya mtaala kwa ujumla, uboreshaji wa mbinu na njia za kufundishia na kujifunzia, mazingira husika, mtaala utaboreshwa kama hautaendana na walengwa.* Mtahiniwa mwingine aliandika hoja za kubuni kama vile: *uhitaji wa watu, mazingira na ukubwa wa watu (ongezeko la watu)* badala ya kuandika hoja sahihi zinazopelekea mabadiliko ya mtaala ambazo ni: *mabadiliko ya falsafa ya nchi, maendeleo ya sayansi na teknolojia, mabadiliko inayoongoza nchi husika, mabadiliko ya mahitaji ya*

*jamii, mabadiliko ya muda* Kielelezo Na. 2.2. ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

| | |
|---|---|
| 2: | 1: Hali duni ya Uchumi wa nchi. |
| | |
| | II: Walimu Ku~~kataa~~ tara mabadiliko ya |
| | mtaala |
| | |
| | III: Vurugu na itikadi za vyama vya |
| | siasa. |
| | |
| | IV: umaskini. |

Kielelezo Na. 2.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 2

Katika Kielelezo Na. 2.2 mtahiniwa aliandika sababu zinazohusu masuala ya uchumi kama vile: uchumi duni, umaskini pamoja na vurugu za kisiasa badala ya kuorodhesha sababu zinazoweza kuleta mabadiliko ya mtaala.

### 2.1.3 Swali la 3: Tathmini katika Elimu

Swali hili lilikuwa na kipengele (a) na (b), ambapo katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kubainisha tofauti mbili kati ya tathmini endelezi na tathmini tamati. Katika kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kuainisha matumizi mawili ya matokeo ya tathmini tamati katika elimu. Jumla ya watahiniwa 2,950 sawa na asilimia 100 walifanya swali hili. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa watahiniwa (94%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 3.




***Chati Na. 3:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa, watahiniwa (6.0%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5, watahiniwa (11.4 %) alama kuanzia 2 had 2.5 na watahiniwa (82.6%) alama kuanzia 3 hadi 4.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 2,437 (82.6%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4 kwa kuwa walikua na maarifa ya kutosha katika mada ya Tathmini katika Elimu. Watahiniwa hawa waliweza kufafanua tofauti kati ya tathmini endelezi na tamati. Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika kuwa: *Tathmini endelezi hufanyika katikati ya mafunzo mfano mitihani ya darasa la nne wakati Tathmini tamati hufanyika mwishoni mwa mafunzo mfano mtihani wa darasa la saba.* Mtahiniwa huyu aliweza kueleza matumizi ya matokeo ya tathmini tamati katika elimu kuwa ni: *hutumika kuboresha mbinu za kujifunzia mfano mbinu shirikishi na hutumika kupata wanafunzi wanaotakiwa kuendelea na ngazi nyingine ya elimu.* Kielelezo Na. 3.1. ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioweza kujibu swali hili kwa usahihi.



| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | (a) | TATHIMINI ENDELEZI | TATHIMINI TAMATI |
| | | i) Hufanyika mara kwa mara wakati wa mafunzo | - Hufanyika mwishoni mwa mafunzo au kozi |
| | | ii) Hulenga kubaini changamoto za wanafunzi, mbinu na njia za kufundishia na hali maye kuboresha. | - Hulenga kutambua changa moto na Uimara wa mtaala wa elimu. |
| | | | |
| | b) | i) Kupata wanafunzi wanao stahili kuendelea nangan nyingine ya elimu | |
| | | ii) Kutambua mafanikio ya mtaala ikilinganishwa na nguvu iliyotumika katika kuwekeza katika elimu. | |

Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 3

Watahiniwa 336 (11.4%) walipata alama kuanzia 2.0 hadi 2.5 kwa sababu walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao kama vile: kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, kutoa majibu pungufu ya yaliyohitajika kwenye swali na kutoa hoja zenye usahihi kidogo, hivyo walipata alama za wastani.

Watahiniwa 177 (6%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Upimaji katika elimu hivyo waliandika majibu yenye mapungufu na yasiyosahihi. Mtahiniwa mmoja alitoa hoja pungufu na zisizosahihi kama vile: *tathmini endelezi ni upimaji ambao bado haujapata taarifa kamili lakini tathmini tamati ni upimaji ambao tayari umepata taarifa.* Mtahiniwa mwingine kati ya hawa alishindwa kutoa tofauti kati ya tathmini endelezi na tathmini tamati ambapo alieleza kuwa: *tathmini endelezi huweza kufanyiwa tatuzi katika ufundishaji na ujifunzaji lakini tathmini tamati haifanyiwi tatuzi katika katika kumsaidia wakati wa mafunzo*. Mtahiniwa mwingine pia alieleza kuwa; *tathmini endelezi hutaka kujua mafanikio au uelewa wa wanafunzi wakati tathmini tamati hutaka kujua mafanikio au changamoto za ujifunzaji.* Watahiniwa hawa badala yake walitakiwa kujikita katika kufafanua tofauti kati ya tathmini endelezi na tathmini tamati pamoja na kuainisha matumizi mawili ya matokeo ya tathmini tamati katika elimu. Kielelezo Na. 3.2. ni sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali hili.

| | | |
|---|---|---|
| 3a. | Tathmini endelezi | Tathmini tamati |
| | Ni tathmini inayotole | Hufanyika baada ya |
| | wa kwa mwalimu | Mchakato wa ufund |
| | na mwanafunzi | ishaji na ujifunzaji. |
| | | |
| | Hufanyika mara | Hufanyika mara moja |
| | kwa mara. | baada ya ufundaji |
| | | |
| | | |
| 3b) | | |

Kielelezo Na. 3.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 3

Katika kielelezo Na.3.2 mtahiniwa hakujibu swali lote pia hakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya tahmini katika elimu. Hivyo alishindwa kujibu swali kwa ukamilifu kuhusu tofauti ya tathmini endelezi na tathmini tamati na kuainisha matumizi mawili ya matokeo ya tathmini tamati katika elimu.

### 2.1.4 Swali la 4: Nadharia za kujifunza

Swali hili lilikuwa na kipengele (a) na (b) ambapo katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kufasili neno kujifunza na katika kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kufafanua kanuni tatu za kujifunza kama zilivyotolewa na mwanasaikolojia Edward Lee Thorndike. Jumla ya watahiniwa 2,950 sawa na asilimi 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa kuwa watahiniwa (67%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 4*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, watahiniwa (33%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5, Watahiniwa (16.4%) alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa (50.6%) alama kuanzia 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 1,693 (50.6%) waliopata alama kuanzia 3 hadi 4 waliweza kufasili neno kujifunza katika kipengele (a) na waliweza kufafanua kanuni tatu za kujifunza kama zilivyotolewa na mwanasaikolojia Edward Lee Thorndike katika kipengele (b). Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Nadharia za kujifunza. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi.



4(a) Kujifunza :- Ni kitendo cha kupata maarifa, muwelekeo na stadi kutoka kwenye mazingira ambalo huleta badiliko la kudumu.

(b) Kanuni tatu za kujifunza ni:-

(i) Kanuni ya Matokeo:- Ni kanuni ambayo huweza kumfanya mwanafunzi kupitia matokeo aliyoyapata kychochea ari ya ujifunzaji na kummotisha mwanafunzi.

(ii) Kanuni ya Mazoezi:- Ni kanuni ambayo hufanyika darasani na kuweza kuongeza ugumu ya kujifunza zaidi.

(iii) Kanuni ya Utayari:- Ni kanuni ya ujifunzaji ambayo mwanafunzi huwa tayari kujifunza kitu ambacho huona kina manufaa kwake.

Kielelezo Na. 4.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 4

Aidha, watahiniwa 483 (16.4%) waliopata alama kuanzia 2 hadi 2.5 walikuwa na maarifa ya kidogo kuhusu dhana ya Nadharia za Kujifunza hivyo Walishindwa kutoa majibu yote kwa usahihi na baadhi yao walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi.

Watahiniwa 974 (33%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5 kwa sababu hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Nadharia za Kujifunza na hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano, alitaja kanuni za kujifunza kwa mujibu wa Edward Lee Thorndike kuwa ni: *kanuni ya utendaji*, *kanuni kabla ya utendaji* na *hatua ya utendaji halisi*. Pia mtahiniwa mwingine alitaja kanuni za kujifunza kuwa ni *kujifunza kwa kuiga* na *kuijfunza kwa kutenda*. Mtahiniwa mwingine pia alitaja kanuni hizo kuwa ni*: kujifunza kwa vitendo, kujifunza kwa miono na kujifunza kwa kuzingatia ushirikiano.* Kimsingi watahiniwa walitakiwa kueleza maana ya kujifunza na kufafanua kanuni tatu za kujifunza ambazo ni: *kanuni ya matokeo, kanuni ya mazoezi na kanuni ya utayari.* Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


4 a) kujifunza: Ni kitendo cha kujua kitu au jambo fulani na kuwoza kulifanyia kazi katika utatuzi wake kwa kulirikiliza au kulcandeka.

4. b) kanuni za kujifunza
i) kuwa makini na mcikivu katika ujifunzaji
ii) kudhukua nukuu juu ya ujifunzaji huo.

Kielelezo Na. 4.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.2 mtahiniwa alieleza mbinu za kujifunza badala ya kanuni za ujifunzaji kama zilivyotolewa na mwanasaikolojia Edward Lee Thorndike.

### 2.1.5 Swali la 5: Saikolojia

Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja sababu zinazowafanya wanasaikolojia kutumia wanyama katika majaribio badala ya binadamu. Jumla ya watahiniwa 2,950 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 71.1 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 5*

Chati Na. 5 inaonesha kuwa, watahiniwa (28.9%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5; watahiniwa (22.8%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa (48.3%) alama kuanzia 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 1,425 (48.3%) waliopata alama kuanzia 3 hadi 4 waliweza kutaja kwa usahihi sababu zinazowafanya wanasaikolojia kutumia wanyama katika majaribio badala ya binadamu. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alitoa hoja kama vile: *kuepuka gharama kwa binadamu, kuepuka vifo kwa binadamu, binadamu hubadilika kulingana na mazingira na wanyama ni rahisi kupatikana katika mazingira halisi.* Watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Saikolojia. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu sahihi katika swali hili.


5.
Sababu zinazowafanya wanasaikolojia kutumia wanyama wanyama katika majaribio badala ya binadamu ni:
- Wanyama wana sika na tabia sawa na binadamu, hivyo ukimfanyia uchunguzi mnyama ni sawa na kumfanyia binadamu
- Binadamu anagharama zaida ya mnyama
- Binadamu anauwezo wa kufikiri na anaakili zaida ya mnyama hivyo anaweza kubadilika.
- Binadamu anaweza kufa na kuonekana kuwa ni ukiukwaji wa haki za binadamu.

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 5

Watahiniwa 673 (22.8%) waliopata alama kuanzia 2 hadi 2.5 walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao ambayo ni: kutoa hoja chache, kuchaganya hoja sahihi na zisizo sahihi na kutoa maelezo yasiyojitosheleza katika majibu hivyo walipata alama za wastani.

Aidha baadhi ya watahiniwa 852 (28.9%) waliopata alama kuanzia 0 hadi 1.5, walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kwa ujumla watahiniwa wengi katika kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sababu zinazowafanya wanasaikolojia kutumia wanyama katika majaribio badala ya binadamu, hivyo walitoa majibu yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alitaja sababu zifuatazo: *idadi ya wanyama, kuomba ridhaa*. Mtahiniwa mwingine alitoa sababu kuwa ni: *wanyama huzaliana kwa wingi, wanyama siyo muhimu sana na wanyama wana kinga za kutosha.* Mtahiniwa mwingine

alitoa hoja kama: *sababu binadamu itachukua masaa mengi katika kuamka, kwa sababu hakuna binadamu yeyote atakaye weza kufanyiwa majaribio, kwasababu hawana ufahamu wowote kuhusu jambo hilo na kwasababu watapunguza ongezeko la binadamu*. Watahiniwa walitakiwa kutaja sababu zinazowafanya wanasaikolojia kutumia wanyama katika majaribio badala ya binadamu kama vile: *kutokiuka haki za binadamu, wanyama hawana gharama kubwa, wanyama wanapatikana kwa urahisi, wanyama wanauwezo wa chini wa kufikiri, wanadamu wanautashi hivyo wanaweza kubadili tabia.* Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


5. i) Binadamu wana uwezo mdogo wa kuta
himili mazingira.
ii) Binadamu akikosa hewa ya oksijeni kwa
muda mrefu anaweza kupoteza fahamu
au kupoteza maisha.
iii) Binadamu ni kiumbe dhaifu.

Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 5

Katika Kielelezo Na. 5.2 mtahiniwa ametoa sababu zinazoeleza zaidi madhaifu ya binadamu badala ya kueleza sababu zinazowafanya wanasaikolojia kutumia wanyama katika majaribio.

### 2.1.6 Swali la 6: Elimu ya watu wazima

Mtahiniwa alitakiwa kubainisha faida nne zinazotokana na mtu mzima kufundishwa kwa kutumia njia shirikishi. Jumla ya watahiniwa 2,950 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa watahiniwa 95.4% walipata alama kuanzia 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 6.




***Chati Na. 6:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6*

Chati Na. 6 inaonesha kuwa watahiniwa (4.6%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5; (6.3%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa (89.1%) alama kuanzia 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi 2,627 (89.1%) waliopata alama kuanzia 3 hadi 4 waliweza kubainisha faida tatu hadi nne zinazotokana na mtu mzima kufundishwa kwa kutumia njia shirikishi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano, alitoa majibu yafuatayo: *kumjengea kumbukumbu ya kudumu au muda mrefu, kumjengea udadisi wa mambo mbalimbali aliyojifunza, kumjengea ujasiri au hali ya kujiamini mbele za watu, kumjengea uwezo wa kujieleza vizuri (kukuza lugha).* Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi.



06 Inasaidia katika utunzaji wa kumbuku
mbu ya kitu alichojifunza

ii) Inamsaidia mtu mzima kuwa na fursa
ya kuuliza maswali kuhusu kile ana
chofundishwa

iii) Inachochea ari ya kuwa mdadisi

iv Inampa mwamko wa mtu mzima wa ku
jifunza kile anachofundishwa

Kielelezo Na. 6.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 6

Baadhi ya watahiniwa 185 (6.3%) waliopata alama kuanzia 2 hadi 2.5, waliandika majibu pungufu ya manne yaliyohitajika kwenye swali na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi.

Aidha watahiniwa 138 (4.6%) waliopata alama kuanzia 0 hadi 1.5 walikuwa na maarifa kidogo kuhusu dhana nzima ya njia shirikishi na hivyo kuorodhesha hoja dhaifu au zisizo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliorodhesha hoja kama vile: *inatumia muda mfupi, inahusianisha mawasiliano baina ya watu wenyewe na zana na inakuza vikundi vya majadiliano*. Mtahiniwa mwingine alitoa faida kuwa ni: *kuwauliza maswali, kupewa motisha na kuheshimiwa*. Aidha, mtahiniwa mwingine alitoa faida hizo kuwa ni: *ili kumsaidia kupata stadi mabalimbali mfano kilimo, ili kumwezesha kupata mbinu au njia za kukabiliana na matatizo mbalimbali.* Kielelezo Na. 6.2. ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



6. – Hurahisisha lengo mahususi kufikiwa.
– Humrahisishia mwalimu ufundishaji
– Humsaidia mwalimu kulimudu ~~darasa~~ somo
– Humsaidia mwalimu kwenda na muda-
sahihi.

Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali 6

Katika Kielelezo Na. 6.2 mtahiniwa alibainisha faida za kutumia zana wakati wa ufundishaji na ujifunzaji badala ya kubainisha faida zinazotokana na mtu mzima kufundishwa kwa kutumia njia shirikishi.

### 2.1.7 Swali la 7: Ufundishaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja mambo manne yanayoweza kuathiri ujifunzaji iwapo wanafunzi watakuwa wengi darasani. Jumla ya watahiniwa 2,950 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwani watahiniwa 51.2% walipata alama kuanzia 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na.7.




***Chati Na. 7:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7*

Chati Na. 7 inaonesha kuwa, watahiniwa (48.8%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5; watahiniwa (29.3%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa (21.9%) alama kuanzia 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 646 (21.9%) waliopata alama kuanzia 3 hadi 4 waliweza kutaja hoja sahihi tatu hadi nne juu ya mambo yanayoweza kuathiri ujifunzaji iwapo wanafunzi watakuwa wengi darasani. Watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Ufundishaji*; hii inatokana na uzoefu walioupata katika mazoezi ya kufundisha kwa vitendo wakiwa mwaka wa kwanza na wa

pili, hivyo walipata alama za juu katika swali hili. Majibu sahihi katika swali hili yalikuwa: *Mwalimu kushindwa kubaini changamoto za wanafunzi na kuwasaidia, wanafunzi kushindwa kuuliza au kujibu maswali yanayoulizwa, wanafunzi waliopo nyuma kushindwa kuona ubaoni, wanafunzi kuwa na miandiko mibaya, wanafunzi kukosa mazoezi au kutokusahihishiwa kazi zao.* Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi.


07 Mambo yanayoweza kuathiri ujifunzaji iwa
po mwanafunzi watakuwa wengi darasa
ni ni
(i) kutofikiwa kwa malengo mahususi kwa
haraka
(ii) ukosefu wa usikivu kwa wanafunzi
(iii) pia huweza kupelekea maendeleo hafifu
ya wanafunzi hao kitaaluma
(iv) Huwa vigumu katika kubaini changamoto
ya kila mwanafunzi darasani

Kielelezo Na. 7.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 7

Kwa upande mwingine, watahiniwa 865 (29.3) waliopata kuanzia alama 2 hadi 2.5 walitaja hoja pungufu ya tatu na baadhi yao walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi.

Baadhi ya Watahiniwa 1,439 (48.8%) waliopata alama kuanzia 0 hadi 1.5 walitaja hoja pungufu ya mbili na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyosahihi hivyo kupata alama za chini. Watahiniwa waliopata alama 0 walitoa hoja zisizosahihi. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu *Dhana ya Ufundishaji*, na hivyo walitoa majibu tofauti na kilichoulizwa. Mtahiniwa mmoja kwa mfano, alitaja hoja kama vile: *miundombinu mibovu, mbinu/njia duni za ufundishaji kwa mwalimu*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama: *hali ya hewa, kukosekana kwa ulinzi na usalama kwa wanafunzi*. Aidha, mtahiniwa mwingine aliandika: *mazingira mabovu/duni, upungufu wa walimu, kutowapa wanafunzi* motisha, *kushindwa kufuata mtiririko mzuri wa maudhui,* Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


7. Mambo manne yanayoweza kuathiri ujifunzaji ni
i) Urithi
ii) Maringira.
iii) Makundi Lika
iv) Magonjwa.

Kielelezo Na. 7.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 7

Katika Kielelezo Na. 7.2 mtahiniwa alitaja mambo ya jumla yanayoweza kuathiri ujifunzaji badala ya mambo mahususi kwa darasa lenye wanafunzi wengi. Aidha, hoja ya kwanza ya urithi haikuhusiana na ufundishaji.

### 2.1.8 Swali la 8: Upimaji katika Elimu

Swali hili lilikuwa na sehemu; (a) na (b) ambapo katika sehemu (a) mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi maana ya upimaji kama inavyotumika katika elimu na kisha aeleze kwa kifupi madhumuni matatu ya upimaji katika elimu. Jumla ya watahiniwa 2,950 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa watahiniwa 99.1% walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Chati Na. 8 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




***Chati Na. 8:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 8*

Chati Na. 8 inaonesha kuwa watahiniwa (0.9%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5; watahiniwa (1.7%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa (97.4%) alama kuanzia 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 2,872 (97.4%) waliopata alama kuanzia 3 hadi 4 waliweza kueleza kwa kifupi kipengele (a); maana ya upimaji kama inavyotumika katika elimu na katika kipengele (b) waliweza kueleza kwa kifupi madhumuni matatu ya Upimaji katika elimu. Watahiniwa hawa wakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana nzima ya Upimaji katika Elimu. Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa na mtahiniwa mmoja ni: *upimaji katika elimu ni kutafuta kiasi gani mwanafunzi amepata maarifa, ujuzi mielekeo, na stadi katika suala zima la mchakato wa kujifunza na kufundisha pia upimaji katika elimu haupimi pekee yake taaluma bali pia hupima mienendo na tabia za wanafunzi.* Katika kipengele (b) mtahiniwa huyu aliweza kueleza kwa kifupi madhumuni matatu ya upimaji katika elimu kuwa ni*; kumsaidia mwalimu kujua matatizo ya wanafunzi katika ujifunzaji wao, kumsaidia mwanafunzi kujenga hali ya kujisomea na ari katika kujifunza kutokana na upimaji na humsaidia mwalimu kuboresha suala zima la mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji.* Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi.


8 a) Upimaji katika Elimu
Ni kitendo cha kuchunguza, kuchambua na kutafu
ni kwa kiasi gani Mwanafunzi amepata Maarifa
ujuzi na stadi kutokana na kile alichofundisha
au kutokana na Mada zilizopo kwenye Muhtasa

b) i) Kuboresha Mbinu na njia za kufundishia
Upimaji husaidia kuboresha mbinu na njia za
kufundishia na kujifunzia.

ii) Kujua Maendeleo ya Wanafunzi kitaaluma.
Upimaji husaidia kujua Maendeleo ya wanafunzi
kitaaluma kutokana na upimaji Mtakao ufanya.

iii) Kujua changamoto zinazowakabili Wanafunzi kati
ujifunza wao. Pia upimaji husaidia kujua ~~Maend~~
changamoto zinazo wakabili Wanafunzi.

Kielelezo Na. 8.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 8

Watahiniwa 50 (1.7%) waliopata alama kuanzia 2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao.

Mapungufu hayo yalikuwa ni: kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi, kurudia hoja na kutoa hoja pungufu ya tatu.

Watahiniwa wachache 28 (0.9%) waliopata alama kuanzia 0 hadi 1.5 walikuwa na maarifa kidogo kuhusu dhana ya *Upimaji katika elimu*. Watahiniwa hawa walitoa hoja pungufu na walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano, alieleza maana ya upimaji kuwa ni: *mchakato au kitendo cha kukusanya, kuchambua na kutafsiri taarifa kwa ajili ya kolewa maamuzi*. Mtahiniwa mwingine alieleza upimaji katika elimu kuwa ni: *mchakato wa kutafuta thamani ya kitu fulani.* Mtahiniwa mwingine alieleza maana ya upimaji kuwa ni: *kitendo cha kupima mchakato wote wa elimu ili kubaini muongozo fulani.* Watahiniwa wengine walitoa majibu yasiyosahihi kama vile: *kutambua matatizo yanayowakabili wanafunz*i, *kujua kama vifaa vya mtaala vinasaidia katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji.* Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


08 upimaji kama unavyotumika katika
elimu; ni mchakato wa kujua maend
eleo ya wanafunzi darasani kadri ufundisha
ji na ujifunzaji unavyoendelea.
b) i) ujuzi wa kuelewa kitu kwa usa
hihi
ii) ujuzi wa kutenda kitu kwa u
fasaha
iii) ujuzi wa kutatua changamoto m
balimbali kwa ufasaha.

Kielelezo Na. 8.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 8

Katika Kielelezo Na. 8.2 mtahiniwa aliandika hoja zinazohusu umuhimu wa kujifunza au kusoma. Mtahiniwa alikuwa na uelewa mdogo kuhusu maana ya upimaji lakini hakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu madhumuni ya upimaji katika elimu.

### 2.1.9 Swali la 9: Uongozi wa Elimu Tanzania

Swali hili lilikuwa na kipengele (a) na (b) ambapo katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kueleza maana ya Uongozi na katika kipengele (b) alitakiwa kueleza kwa kifupi mambo matatu yanayotokana na uongozi uliobweteka katika shule za msingi. Jumla ya watahiniwa 2,950 sawa na

asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa watahiniwa 92.3% walipata alama kuanzia 2 hadi 4 kama inavyooenekana katika Chati Na. 9.




***Chati Na. 9**: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 9*

Chati Na. 9 inaonesha kuwa watahiniwa (7.7%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5, watahiniwa (11.4%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa (80.9%) alama kuanzia 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 2,385 (80.9%) waliopata alama kuanzia 3 hadi 4 waliweza kueleza maana ya Uongozi na kueleza kwa kifupi mambo mawili hadi matatu yanayotokana na uongozi uliobweteka katika shule za msingi. Watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ndogo ya *Dhana ya Uongozi wa Elimu.* Mtahiniwa mmoja kwa mfano katika kipengele (a), alitoa maana ya uongozi kuwa ni: *mamlaka anayokuwanayo mtu ya kusimamia mambo mbalimbali mfano kusimamia utekelezaji wa mtaala.* Katika kipengele (b) mtahiniwa alitoa hoja kama vile: *kucheleweshwa kwa maendeleo katika shule, watu kutowajibika ipasavyo, na wanafunzi kutofanya vizuri katika masomo.* Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya majibu sahihi katika swali hili.



Kielelezo Na. 9.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 9

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 337 (11.4%) waliopata alama kuanzia 2 hadi 2.5 walitaja hoja pungufu au walirudia hoja zaidi ya mara moja. Aidha katika kundi hili kulikuwa na watahiniwa waliochanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na hivyo walipata alama za wastani.

Kwa upande mwingine watahiniwa 228 (7.7%) waliopata alama kuanzia 0 hadi 1.5; wengi wao waliweza kueleza maana ya uongozi. Aidha, katika kipengele (b), baadhi yao walitoa hoja pungufu ya mbili na wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya *Uongozi wa Elimu.* Mtahiniwa mmoja kwa mfano alieleza mambo matatu yanayotokana na uongozi

uliobweteka katika shule za msingi kuwa ni: *uwepo wa mwenyekiti wa shule, ushirikishwaji wa jamii kupitia kamati ya shule na kushirikisha wazazi katika mambo ya shule.* Mtahiniwa mwingine alitoa majibu kama vile: *uongozi usiofuatiliwa, uongozi unaopokea maamuzi kutoka juu ya uongozi wa juu na uongozi unaohitaji maelekezo kutoka kwa kiongozi husika*. Aidha mtahiniwa mwingine alieleza mambo hayo kuwa ni: *urafiki, kuogopa migogoro* na alishindwa kueleza maana ya uongozi. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


9a) Ni kile ktendo cha watu kufanya ma
amuzi ya kumchagua au kuchagua baadhi
ya watu wawaongoze wao.
b) i) Wanafunzi kutokuwa na uelewa juu ya uongozi
ii) Wanafunzi wa shule ya msingi bada hawa
jawa na ule uwezo mkubwa wa kufikiri hivyo ku
chukulia nafasi za uongozi walizopewa kuwna
ni kawaida tu.
iii) Waalimu kutowapa wanafunzi wao elimu ina
yohusiana na uongozi

Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 9

Katika Kielelezo Na. 9.2 mtahiniwa alielezea zaidi uelewa mdogo wa wanafunzi katika masuala ya uongozi badala ya kuelezea maana ya uongozi na mambo matatu yanayotokana na uongozi uliobweteka katika shule za msingi.

### 2.1.10 Swali la 10: Matayarisho ya Ufundishaji

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kwa kutumia hoja nne kuwa ni muhimu kufanya majaribio ya zana au vifaa vya kufundishia na kujifunzia somo la Sayansi kabla ya kuvitumia darasani. Jumla ya watahiniwa 2,949 sawa na asilimia 99.97 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa watahiniwa 94.8% walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Chati Na. 10 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 10*

Chati Na. 10 inaonesha kuwa, watahiniwa (5.2%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5, watahiniwa (9.0%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa (85.8%) alama kuanzia 3 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi 2,531 (85.8) waliopata alama kuanzia 3 hadi 4 walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya matayarisho ya ufundishaji. Watahiniwa hao waliweza kutoa hoja tatu hadi nne kuthibitisha kuwa ni muhimu kufanya majaribio ya zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia somo la Sayansi kabla ya kuvitumia darasani. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya watahiniwa katika swali hili.


10. i) Husaidia kuepusha ajali zinazoweza kutokea wakati wa kutumia zana kama ili kuwa ni mbovu

ii) Ili kujua ubora wa zana

iii) Ili kujenga uzoefu wa kuitumia

iv) Ili kufanya maboresho kabla ya kuitumia

Kielelezo Na. 10.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 10

Watahiniwa 266 (9.0%) waliopata alama kuanzia 2 hadi 2.5, walitoa hoja pungufu na wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi hivyo kupata alama za wastani.

Watahiniwa 152 (5.2%) waliopata alama 0 hadi 1.5 hawakuwa na maarifa ya kutosha katika dhana husika na hivyo kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Wengine walitoa majibu yote yasiyo sahihi kutokana na kutokuwa na maarifa kuhusu Dhana ya *Matayarisho ya Ufundishaji*. Mmoja wa watahiniwa alitoa hoja kama vile: *zana/vifaa humsaidia mwanafunzi katika kumjengea kumbukumbu za kudumu, zana/vifaa humsaidia mwalimu katika kufikiwa kwa malengo aliyokusudia au mahususi*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile: *zana/vifaa ni lazima iwe na ukubwa wa wastani na unaobebeka kwa urahisi, zana vifaa iendane na mada inayofundishwa, au itakayofundishwa, na somo, zana lazima iwajengee wanafunzi kumbukumbu*. Pia mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile: *ili kubaini iwapo zana hizo zimekidhi vigezo vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu, ili kubaini kama zana hizo zitachochea udadisi kwa wanafunzi na ili kubaini kama zana hizo sio za kuogofya.* Majibu haya ya watahiniwa hayakuwa sahihi kwani *walitakiwa* kutoa hoja zinazohusu umuhimu wa kufanya majaribio ya zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia kabla ya kuvitumia darasani katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Sayansi. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



10. Zana/vifaa - Hivi ni vifaa ambavyo mwalimu anavitumia katika swala zima la kufundisha na kujifunzia zana hizi zinaweza zikawa halisi au zisiwe halisi kulingana na mazingira.

Ni kweli kabisa kuwa katika hali ya kufundisha na kujifunza upo umuhimu wa kutumia zana umuhimu huu ni pamoja na.

Zana inamfikirisha mwanafunzi, ni kwasababu mwanafunzi anapo ona zana basi atafikiri sana juu ya umahili na stadi zilizo tumika kwandaa zana hiyo.

Inamfanya mwanafunzi kulipenda somo, kutokana na zana kumuntia mwanafunzi basi atalipenda somo na kulifatilia kwa undani zaidi hivyo waalimu tujitaidi kuboresha zana zetu.

Inamfanya mwanafunzi kuwa mdadisi, hapa atajaribu kudadisi na kujiuliza maswali ya fwatayo "kwanini?" na kumfanya ajaribu pia.

Inasaidia kuvuta umakini wa mwanafunzi, kutokana na zana nzuri basi mwanafunzi atakuwa makini katika kujifunza.

hivyo, zana ni muhimu katika swala zima la kujifunza.

Kielelezo Na. 10.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 10

Katika Kielelezo Na. 10.2 mtahiniwa alitoa hoja zinazoelezea zaidi umuhimu wa kutumia zana wakati wa kufundisha na kujifunza darasani badala ya kutoa hoja zinazoonesha umuhimu wa kufanya majaribio ya zana au vifaa vya kufundishia na kujifunzia somo la Sayansi kabla ya kuvitumia darasani.

## 2.2 SEHEMU B: Saikolojia ya Elimu

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ya insha, swali la 11 na swali la 12. Kila swali lilikuwa na alama 15, Watahiniwa walitakiwa kijibu swali 1.

### 2.2.1 Swali la 11: Saikolojia

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuchambua kwa kina vipengele sita vya Nyanja ya utambuzi na kisha kutunga swali moja kwa kila kipengele. Jumla ya watahiniwa 1,123 sawa na asilimia 38.1 ya watahiniwa waliofanya

mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 93% walipata alama kuanzia 6 hadi 14. Chati Na.11 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




***Chati Na. 11:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11*

Chati Na. 11. Inaonesha kuwa, watahiniwa (7.0%) walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5, watahiniwa (69.1%) alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa (23.9%) alama kuanzia 10.5 hadi 15. Aidha, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulianzia alama 0 hadi 14.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 268 (23.9%) waliopata alama kuanzia 3 hadi 4 waliweza kuchambua vipengele sita vya Nyanja ya utambuzi na kisha kutunga swali moja kwa kila kipengele kwa usahihi. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu Nyanja ya utambuzi katika utunzi wa maswali. Wengi kati yao walianza na utangulizi uliojitosheleza na maelezo sahihi ya kutetea hoja zao. Kielelezo Na. 11.1 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi.

11. Nyanja ya utambuzi ni nyanja inayotumika kupima ujuzi na uzoefu aupatao mwanafunzi katika kujifunza. Nyanja ya utambuzi ni nyanja muhimu ya kuzingatia wakati wa kupima stadi, ujuzi na mielekeo mbalimbali. Nyanja hii ni muhimu kwa sababu humjengea mwanafunzi uwezo wa kukumbuka, kujieleza, kupambanua mawazo na kufikiri kwa kina katika kutafuta maarifa aliyofundishwa. Nyanja ya utambuzi ina vipengele sita (6) ambavyo hupimwa. Vifuatavyo ni vipengele hivyo.

Maarifa, hutumika kupima uwezo wa mwanafunzi wa kukumbuka taarifa (maarifa) aliyofundishwa au kujifunza darasani. Ngazi hii ni muhimu kwani humwezesha mwanafunzi kurudisha wazo au maarifa aliyojifunza. Mfano wa katika kipengele hiki ni "Taja njia mbili za kudhibiti ongezeko kubwa la idadi ya watu katika maeneo".

Ufahamu, katika kipengele hiki mwanafunzi hupima na kuonesha mambo yanamfanya aoneke na anafahamu jambo fulani na anaweza kulielez na kulipangilia kwa ufasaha. Mfano wa swali katika kipengele hiki, "Onesha jinsi kupatwa kwa jua kunavyotokea."

Matumizi, katika kipengele hiki swali humtaka mwanafunzi atumie habari aliyoisoma au




Kielelezo Na. 11.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 11

Watahiniwa 779 (69.1%) waliopata alama kuanzia 6 hadi 10 katika swali hili, walikuwa na maarifa kiasi katika swali hili, kwani walitoa maelezo yenye usahihi kwa kiasi fulani katika kueleza hoja zao. Watahiniwa hao waliweza kuainisha vipengele vya nyanja ya utambuzi na kutunga swali kwa kila kipengele ingawa walionesha kuwa na mapungufu mbalimbali katika insha zao kama kwenye utangulizi na hitimisho ambavyo havikujitosheleza na kushindwa kutunga maswali yanayoendana na vipengele vya Nyanja ya utambuzi.

Kwa upande mwingine watahiniwa 79 (7.0%) waliopata alama kuanzia 0 hadi 5.5 hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vipengele vya nyanja ya utambuzi, hivyo walitoa majibu pungufu, walichanganya vipengele na

walishindwa kutunga maswali kwa kila kipengele. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alitaja vipengele vya Nyanja ya utambuzi kuwa ni: *utendaji* na swali alilotunga katika kipengele hiki ni *ukiamka asubuhi unafanya kitu gan*i. Mtahiniwa mwingine kati ya hawa alichanganya vipengele sahihi na visivyo sahihi vya Nyanja ya utambuzi kama ifuatavyo: *maarifa, uundaji, matumizi, uunganishaji, utendaji na tathmini.* Mtahiniwa mwingine alitaja vipengele vya nyanja ya utambuzi kuwa ni: *uthamini, utayari* na katika nyanja ya uthamini alieleza kuwa: *uthamini hupima mwanafunzi jinsi ya kujithamini na kuthamini. Mfano wa swali linaloweza kuulizwa ni eleza umuhimu wa afya bora*. Watahiniwa walitakiwa kutoa majibu kwa mpangilio katika kuelezea vipengele vya nyanja ya utambuzi ambavyo ni: *maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji, na tathmini*. Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kukidhi matakwa ya swali katika swali hili.

11. a) Uchambuzi wa Maswali.

(i) Nishati Maswali 6

(ii) Afya Maswali 6

(iii) Mazingira Maswali 5

(iv) Uchunguzi wa kisayansi Maswali 3

(b) Maarifa Maswali 3

Ufahamu Maswali 3

Matumizi Maswali 4

Uchambuzi Maswali 3

Uundaji Maswali 4

Tathmini Maswali 3

Jumla ya Maswali 20

Maswali rote 100%.

| Mada kuu | Mada Ndogo | Shughuli zinazojanyiwa upimaji | | | | | | Jumla | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Maarifa | Ufahamu | Matumizi | Uchambuzi | Uundaji | Tathmini | | |
| Nishati | | 1 | | 2 | 1 | 2 | | 6 | 30% |
| Afya | | | 2 | 1 | 1 | 1 | 1 | 6 | 30% |
| Mazingira | | 1 | 1 | | 1 | | 2 | 5 | 25% |
| Uchunguzi wa kisayansi | | 1 | | 1 | | 1 | | 3 | 15% |
| Jumla | | 3 | 3 | 4 | 3 | 4 | 3 | | |
| Asilimia | | 15% | 15% | 20% | 15% | 20% | 15% | | 100% |

Kielelezo Na. 11.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 11

Katika Kielelezo Na. 11.2 mtahiniwa alichora jedwali la utahini badala ya kuchambua na kutunga maswali kwenye vipengele sita vya nyanja ya utambuzi kwa usahihi kama vilivyofafanuliwa na Benjamin Bloom.

### 2.2.2 Swali la 12: Makuzi na Ukuaji wa Mtoto

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja sita kueleza jinsi mazingira yanavyoweza kuathiri ukuaji wa mtoto aliye tumboni kwa mama. Jumla ya watahiniwa 1,825 sawa na asilimia 61.9 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa (96.9%) ya watahiniwa walipata alama kuanzia 6 hadi 14.5 kama inavyoonekana katika Chati Na. 12.




***Chati Na. 12:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 12*

Chati Na. 12 inaonesha kuwa, watahiniwa (3.1%) walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5, Watahiniwa (19%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa (77.9%) alama kuanzia 10.5 hadi 15. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulianzia alama 0 hadi 14.5.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa wengi 1,422 (77.9%) waliopata alama 10.5 hadi 14.5 walikuwa na uelewa mpana kuhusu ukuaji wa mtoto. Watahiniwa hawa waliweza kutumia hoja sita kueleza jinsi mazingira yanavyoweza kuathiri ukuaji wa mtoto aliye tumboni kwa mama. Majibu sahihi katika swali hili yalikuwa: *matumizi ya madawa ya kulevya, ajali, chakula duni, matumizi ya pombe na maradhi kama vile kisonono na*

*kaswende, mionzi na uvutaji sigara.* Kielelezo Na. 12.1 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi.



12: Mazingira ni kitu chochote kinachomzunguka binadamu mazingira yanaweza kuathiri ukua wa mtoto aliye tumboni mwa mama kwa mambo mbali zipo yazingatia na kuyatilia mkazo. Zifuatazo ni namna au jinsi mazingira yanayoweza kuathiri Ukuaji wa mtoto aliye tumboni:-

Lishe duni: lishe duni ni mojawapo ya mazingira yanayoweza kuathiri mtoto tumboni kwa mama hasa pale anapokosa virutubisho muhimu vya chakula vinayoweza kumsaidia mama mjamzito na kumlinda mto tumboni. hivyo lishe inawezo kusababisha athari kubwa ya Ukuaji wa mtoto tumboni kwa mama:

Magonjwa: pia magonjwa yanaweza kusababisha ukuaji wa mtoto kwa hapizu tumboni na hivyo kupelekea kuzaliwa mtoto mwenye ulemavu wa ubongo au viungo vingine vya mwili mfano wa magonjwa hayo ni hasa magonjwa ya ngono na Ukimwi pia huweza kusababisha ukuaji hafifu wa mtoto tumboni

Matumizi ya madawa ya kulevya: matumizi ya madawa ya kulevya pia kinaweza kwa ni chanzo cha mazingira hatarishi kwa mtoto aliyetumboni mfano matumizi ya pombe kali, kokeini na bangi vinaweza kuathiri Ukuaji wa mtoto aliye tumboni kwa mama.



12: Matatizo ya kisaikolojia: pia matatizo ya kisaikolojia kama vile msongo wa mawazo unaweza kupelekea ukuaji hafifu wa mtoto tumboni-hii ikiwa na maana kwamba, mama akiwa na mawazo mengi anaweza kuathiri ukuaji wa mtoto tumboni.

Mama kutumia pombekali, Uvutaji wa sigara na Umalaya: Haya pia ni mazingira ambayo ni hatarishi kwa mama mjamzito kumu sigara na Uasherati unaweza kumuathiri mto tumboni. Hiyo haya pia ni mazingira yanay owezo kusababisha mtoto tumboni kuathirika.

Mama mjamzito kukosa matibabu. Mam mjamzito anapaswa kupata matibabu ya mar kwa mara ili kujua maendeleo ya mtoto tumb oni hiyo kama akikosa matibabu maja kwa mga anaweza kupelekea mtoto aliyepo tumboni kuathirika.

Hiyobasi mama mjamzito anapaswa kuwa na mazoea ya kwenda kliniki ya mimba ili kupata matibabu na kujua maend eleo ya mtoto tumboni, kule chakula bora yenye kishe, kuepukana na misongo ya ma wazo na kuepukana na uvutaji bangi, mad awa ya kulewa na Umalaya: kwa kufanya haya mtoto aliye tumboni anaweza kukua kama mazingira mazuri na salama.

Kielelezo Na. 12.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 12

Watahiniwa 347 (19%) walipata alama za wastani katika swali hili, kwa kuwa walishindwa kutoa maelezo sahihi katika kueleza hoja zao au walishindwa kuandika utangulizi na hitimisho linalojitosheleza. Miongoni mwa watahiniwa hawa wapo waliochanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na hivyo kupata alama pungufu.

Aidha, watahiniwa 56 (3.1%) waliopata alama hafifu katika swali hili, walikuwa na uelewa mdogo kuhusu ukuaji wa mtoto na hivyo kutoa hoja

zenye usahihi kidogo sana na wengine kati yao waliandika hoja bila ufafanuzi ulio jitosheleza, vilevile hawakuwa na utangulizi au hitimsisho zuri. Watahiniwa wengine katika kundi hili hawakuwa na maarifa kabisa kuhusu dhana ya *makuzi na ukuaji wa mtoto* hivyo walitoa majibu tofauti na dhana iliyoulizwa. Mtahiniwa mmoja kwa mfano, aliandika hoja zifuatazo: *mtoto anaweza kurithi tabia ya mama, mtoto huweza kuzaliwa na ulemavu, mtoto huweza kukosa stadi mbalimbali, mtoto huweza kukosa lishe bora, mtoto huweza kukosa baadhi ya mila na desturi, mtoto anaweza kuathirika kisaikolojia*. Mtahiniwa mwingine aliandika hoja kama vile: *ukame, umaskini imani za kishirikina, mila na desturi potofu*. Watahiniwa wengine walieleza hoja kama: *mazingira humfanya mtoto kuvia kiakili, mtoto kuzaliwa na viungo pungufu vya mwili, kuharibika kwa mimba, mtoto kuzaliwa na afya duni na mtoto kuzaliwa na magonjwa*. Badala yake watahiniwa walitakiwa kutaja na kuelezea hoja kama vile: *lishe duni, matumizi ya madawa ya kulevya, matumizi ya mionzi, matumizi ya pombe kali, magonjwa ya ngono, uvutaji wa sigara* na *matumizi ya madawa ya hospitalini*. Kielelezo Na. 12.2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu swali kwa usahihi.

12 Mazingira nijumula ya Vitu vyote vina
vyo mzunguka Muwanda mi kalika maisha
yakaya kila siku. mazingira ya weza ku
jumusha Viumbe hai na Visivyo hai mfano
milima na hata minuea na wanyama
wengine. Pia mazingira ya weza kuhus
ha makazi yetu.
Zifuatazo ni Sababu ambazo zina
weza kuathiri makuzi ya Mtoto aliye
kuwa tumboni kutokana na mazingira:
Mtoto kushindwa kukua vizuri Pindi aki
wa tumboni Mwamama, kimsingi hii husa
babishuwa na Chakula amba cho mama
anakula akuwa mjumzito kutokana na
mazingira anayo ishi mfano kutokula
Chakula cha kufanya Mtoto akuwe viz
uri ya chakula protini kama vile maya
i na hata karanga.
Mtoto kuzaliwa akuwa na ulemavu wa
vungo, Hii hutokana na matumizi ya ma
dawa ya kulevya ambayo ya
weza ku haribu mfuno wa homo ka
hatu za ukuwaji wa Mtoto tumboni mfa
vidonge vya majira
Mtoto kuzaliwa akuwa na Mtindio
wa ubongo, Hii hutokana na kupata
ajari mbalimbali kuwa mama mia m



12 Zito na kunfanya mtoto apate mtikisi
ko wa ubongo hivyo kunfanya mto
toto kuwa na mtandio wa bongo swa
la ambalo linaweza kumuathiri ka
tika shughli za ujifunza mfano ajari
ya gari mama kuanguka kwa kahat
imbaya.
Mtoto kuzaliwa na tabia zenye hasira,
Pia hiu hitolana na mchusano ma
baya ya mama na jamii inayom
zuinguka kwa kuishi kwa tabia za
asira swala ambalo linaweza kufanya
mtoto na yeye awe na hasira;
Mtoto kuzaliwa akuwa na udimavu
katika kukua kwake, Pia hiu husabu
bisuwa na mama kutofuata hatu zilizo
thabiti kipindi cha mimba amaaya
uzito mfano kutohuthuria kihingi.
Mtoto kuzaliwa na udhofu wa mwili
Hupia inaweza ikasababisuwa na malazi
ya mama katika mazingira yake na us
afi wa mwa katika swala zima la cha
kula anado kula kulo kwa kisafi
Hivyo basi mazingi ni la zima
yauwe rafiki kuwa nia ya kufa
nya mtoto awe salama pamojana
ukuaji wake. mpaka anapozalia
wa kwa kuuhida mama mjamzito.

Kielelezo Na. 12.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 12

Katika Kielelezo Na.12.2 mtahiniwa alijikita zaidi katika kueleza madhara anayoweza kupata au anayopata mtoto kutoka kwa mama mjamzito badala ya kuelezea jinsi mazingira yanavyoweza kuathiri ukuaji wa mtoto aliye tumboni mwa mama.

## 2.3 SEHEMU C: MITAALA NA UFUNDISHAJI

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (2) ya kujieleza; swali la 13 na 14. Kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15). Watahiniwa walitakiwa kujibu swali moja.

### 2.3.1 Swali la 13: Ufundishaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza faida tatu na hasara tatu za njia ya maswali na majibu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Jumla ya watahiniwa 617 sawa na asilimia 20.9 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa (91.6%) ya watahiniwa walipata alama kuanzia 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 13.




***Chati Na. 13:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 13*

Chati Na. 13 inaonesha kuwa watahiniwa (8.4%) walipata alama kuanzia 0.0 hadi 5.5, Watahiniwa (71.8%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa (19.8%) alama kuanzia 10.5 hadi 15. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulianzia alama 2.5 hadi 14.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 122 (19.8%) waliopata alama kuanzia 10.5 hadi 14 walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu faida na hasara za njia ya maswali na majibu. Watahiniwa hawa waliweza kueleza faida tatu na hasara tatu za njia ya maswali na majibu

kwa usahihi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliopata ufaulu mzuri katika swali hili.



13 Njia ya maswali na majibu hii ni
mojawapo ya mbinu shirikishi ambay
mwalimu anaweza kuitumia katika uf
undishaji wake ndani ya darasa kwa
kumuuliza mwanafunzi swali na mwanafunz
kujibu hapo kwa hapo'
Zifuatazo ni faida na hasara za
kutumia mbinu ya maswali na majabi
wakati wa ufundishaji.
kwa kuanza na ~~hasara~~ faida
za mbinu hii
huvuta usikivu na umakini, m
walimu anapotumia mbinu hii humsaidi
a mwanafunzi awe msikivu na akaema
kini endapo ataulizwa swali aweze
kulimudu swali na kulijibu vilevile
itamplekea awe makini kusikiliza maji
bu ya wenzake kwa umakini ili aep
uke kurudia makosa ya wenza ke
Mfano Raisi wa Tanzania ni" hapa
atavuta umakini na kukumbuka.
Humfanya mwanafunzi kulipenda na
kulifurahia somo, vilevile mbinu hii
huleta changamoto na ushindani nda
ni ya darasa hivyo kila mwanafunzi
akupata nafasi ya kujibu na akajibu vye
ma hii itampelekea apende kujifunza
apende somo na kupenda kusoma
kwa bidii ili aweze kupata stadiza'
kujibu maswali na kuwashinda wenzake
na ni fahari kwa mwanafunzi mbele ya
wenzie kujibu maswali

13. Humrahisishia mwalimu ufundishaji pia hukuza ushirikiano ndani ya darasa, vilevile Mwalimu anapotumia mbinu ya maswali na majibu hii humsaidia kuimrahisishia ufundishaji kwani kazi yake itakuwa ni kuandaa tu maswali ambayo ya fasibiwa na wanafunzi pia ukukuza ushirikiano kati ya mwalimu na mwanafunzi na mwanafunzi na mwanafunzi

Vilevile zifuatazo ni hasara za kutumia mbinu ya maswali na majibu

Isipo tumika vizuri huweza kusababisha makelele, darasani mwalimu aspotumia mbinu hii kwa mpangilio mzuri inaweza kusababisha kelele kwani kila mwanafunzi atataka kujibu swali hivyo ni vyema mwalimu kutumia utaribu mzuri mfano wanafunzi kuki mbilia mbele ya ubao'

Hutumia muda mwingi, katika kuandaa maswali vilevile katika kuuliza hii hutumia muda mwingi hivyo kwa kipindi cha dakika 40 ni ngumu kwa mwalimu kuuliza maswali mengi na kuyafanyia masahihisho hivyo inapaswa mwalimu afanye maandalizi mazuri na kuweko muda wa kujibu kila swali mfano kila swali litatumia dakika moja (1) katika ujibuji wake pasipo na hapo mbinu hii inaweza isiwe rafiki sana.



13 Inaweza isishirikishe wanafunzi wote
pia inaweza ikasababisha upendeleo, vilevi
le katika kutumia mbinu hii mwa
limu asipokuwa makini anaweza ku
sababisha kutoshirikisha wanafunzi wote
kwani atakuwa akiuliza ~~wana~~ baadhi
ya wanafunzi tu na hiyo ikapelekea
upendeleo'
Hivyo basi, ili mwalimu aweze
kufanikiwa ni lazima atumie mbinu
nyingi katika kupindi kimoja mfano onye
sho mbinu, fikirisha, jozisha, shirikisha pia
matumizi ya zana ni muhimu sana. ~~na~~

Kielelezo Na. 13.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 13

Kwa upande mwingine watahiniwa 443 (71.8%) waliopata alama kuanzia 6 hadi 10.5 walikuwa na ufaulu wa wastani katika swali hili kwa sababu baadhi yao waliweza kutoa utangulizi sahihi lakini walishindwa kuchambua vizuri hoja zao na wengi wao walitoa hoja pungufu hivyo kupata ufaulu wa wastani.

Aidha, watahiniwa 52 (8.4) waliopata alama kuanzia 2.5 hadi 5.5 hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya ufundishaji hivyo walichanganya majibu sahihi na yasiyosahihi. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alitoa hasara ya mbinu ya maswali na majibu kuwa ni: *kupelekea kelele darasani, mwalimu kushindwa kujua kama wanafunzi wote wameelewa kilichofundishwa.* Mtahiniwa mwingine alitaja faida ya njia ya maswali na majibu kuwa ni: *humsaidia mwalimu kufundisha somo kwa kujiamini,* na hasara ni *ngumu au vigumu kufikia malengo na rahisi kutoka nje ya mada.* Katika hoja ya "rahisi kutoka nje ya mada" mtahiniwa alifafanua kuwa *unapotumia njia hii ya maswali na majibu, majiibu mengine huitaji kutoka nje ya mada ili mwanafunzi akuelewe.* Mtahiwa mwingine alitaja hasara ya njia ya maswali na majibu kuwa ni*: wanafunzi kushindwa kujua au kuelewa lengo kuu la mada wanayojifunza, ni rahisi kwa wanafunzi kusahau walichouliza au walichojibu kutokana na swali waliloulizwa na wanafunzi kuuliza maswali ya nje ya mada:* Kielelezo Na. 13.2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

| | |
|---|---|
| 13 | Inasaidia kumotisha wanafunzi |
| | na kukuza ari ya kuipenda |
| | somo ; hii ni kutokana na |
| | ujibuji wa maswali yaliyotolewa |
| | Mtano Mwanafunzi kafanya |
| | vizuri au kajibu vizuri na |
| | kuwa ufawaha alafu Mwalimu |
| | akampa tiki na kumuandikia |
| | vizuri, vizuri sana hii humfaya |
| | Mwanafunzi kupenda somo na |

[redacted]

13 Hupelekea ubaguzi na Matabaka darasani; au katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, kutokana na njia hii ya Maswali na Majibu inapofanyika na mwalimu Mfano ukatoa swali darasani na wanafunzi wakafanya vizuri zaidi, vizuri na wengine wamejitahidi ila mwisho wa siku daraja lina kua na Matabaka ya wale wanaofanya vizuri, wanaofanya vizuri zaidi na wanaojitahidi na kusababisha kutengana.

Inapelekea Mwanafunzi kuanza utoro au kuacha shule kabisa; hii ni kutokana na njia hii inapotumika pale panapoanza Matabaka hupelekea Mtu au Mwanafunzi kuona kama anatengwa na kuacha shule au Mwanafunzi kuanza utoro kwasababu ajifanya kazi ya mwali au hajajibu maswali aliyopewa hakini pia Mwanafunzi kuona yeye ni mchahifu katika somo hilo na kujiona hawezi na atimaye kuacha shule.



13 Inasababisha Maadili ya
wanafunzi kushuka na kuharibika
hii ni kutokana na Maswali
kujibiwa kwa ufasaha zaidi,
kwa ufasaha na kwa udhaifu:
hii hupelekea mwanafunzi
kwa na tabia mbaya mfano
kuigia kwenye chumba cha
mtihani au kuigia ujibuji au
kuigia majibu na hata aliye
fanya vibaya akaacha shule
na kubaki mtaani bila elimu
na kuishia kuwa muizi, kibaka
mlevi na vinginevyo.
Hivyobasi katika kila kitu
kuna faida na hasara zake
mbinu hii au njia hii ya
maswali na majibu humsaidia
mwalimu kubaini kama malengo
yamefikiwa lakini pia je!
kama hayajafikiwa na mgharimu
kupoteza muda na kujitolea
muda wa ziada kurudia, ila
asingetumia asinge baini na
kupoteza muda wa kufundisha
mada kuu au mada nalogo
hucika.

Kielelezo Na. 13.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 13

Katika Kielelezo Na. 13.2 mtahiniwa aliweza kuandika hoja moja sahihi kuhusu faida ya njia ya maswali na majibu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ambayo ni kuwamotisha wanafunzi na kukuza ari ya kupenda somo. Hoja nyingine zote hazikuhusiana kabisa na faida au hasara za njia ya maswali na majibu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.3.2 Swali la 14: Ufundishaji

Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua faida sita za kutumia njia ya majadiliano ya vikundi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Jumla ya watahiniwa 2,336 sawa na asilimia 79.2 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri

kwa kuwa, watahiniwa 99.7% walipata alama kuanzia 6 hadi 15. Chati Na. 14 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 14.




***Chati Na. 14:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 14*

Chati Na. 14 inaonesha kuwa watahiniwa (0.3%) walipata alama kuanzia 0.0 hadi 5.0, watahiniwa (33.9%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa (65.8%) alama kuanzia 10.5 hadi 15. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulianzia alama 4.5 hadi 15.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi 1,538 (65.8%) waliopata alama kuanzia 10.5 hadi 15, waliweza kufafanua faida sita za kutumia njia ya majadiliano ya vikundi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa hawa pia walikuwa na uwezo mkubwa katika uandishi wa insha kuanzia utangulizi hadi kwenye hitimisho. Baadhi ya hoja zilizotolewa na watahiniwa katika swali hili ni pamoja na; *humfikirisha mwanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, kukuza stadi ya kujieleza, husaidia kukuza stadi ya udadisi, huleta ushindani wa kujifunza kati ya wanafunzi kwa wanafunzi, husaidia wanafunzi kuwa na ushirikiano.* Kielelezo Na. 14 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi.

14 Majadiliano; Ni kitendo cha kuwapo nga watu katika makundi kwa lengo-la kujadili kutokana na mada husika-ili kufikia malengo katika swala zima-la ufundishaji na ujifunzaji. zifuatazo ni faida za kutumia mbinu ya majadili-ano ~~kta~~ ya vikundi katika mchakato ufun-dishaji na ujifunzaji. ambazo ni.

Inamjengea mwanafunzi kumbu-kumbu. Hii ni kweli kwamba mwalimu atumiapo mbinu ya majadiliano katika tendo zima la ufundishaji inamjengea mwanafu-nzi kumbukumbu kwa sababu inamfikiri-sha wakati akiwa katika kundi na kum-fanya asisahau kamwe.

Inaibua udadisi; pia pindi m-walimu anapo tumia mbinu ya majadilia-no ya vikundi kwa wanafunzi hui bua-udadisi na kuuliza maswali tofauti tofa-uti wakati akiwa kwenye kundi napindi anapo wasilisha mawazo yake. na mwingi-ne wa kundi lingine kutokana majibu-aliyoyapata wakiwasilisha wana wafanyo wengine waibue udadisi.

Inamfikirisha mwanafunzi. pia-mbinu hii humfanya mwanafunzi afikiri kwa kina juu ya jambo ambalo anali-jadili katika kundi na wenzake itamfa-nya awe na uwezo mkubwa wa kufikiri-na kuwezo kupambanua mambo na kuya-pata majibu. kwa sababu atafikiri sana hadi apate jibu hivyo ita kuza uelewa wake

14 ~~Hu~~ Inamjengea mwanafunzi kujiamini.
Hii ni kweli kwamba mwalimu pindi ana
potumia mbinu ya mjadiliano kufundishi
a inamfanya mwanafunzi ajiamini na

Kielelezo Na. 14.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 14

Watahiniwa wengi 792 (33.9%) waliopata alama za wastani katika swali hili, walitoa hoja pungufu na baadhi ya maelezo yao hayakuwa na uhusiano na swali. Wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi.

Watahiniwa wachache (0.3%) walipata alama kuanzia 4.0 hadi 5.0. Baadhi yao walikuwa na maarifa kidogo kuhusu dhana ya ufundishaji na hivyo waliweza kuandika angalau utangulizi na hoja chache ambazo walishindwa kuzielezea, hivyo walipata alama za chini. Mtahiniwa mmoja kwa mfano aliandika hoja kama: *uburudisha, husaidia katika utoaji wa jibu moja, husaidia katika kuongeza maarifa*. Mtahiniwa mwingine alielezea hoja kama: *kuwa na maamuzi ya busara kwasababu kila mwanafunzi huweza kufikiri kwa kina na kutoa mawazo ili kuweza kupata wazo kuu moja.* Hoja nyingine aliyoitoa ni: *huwajea ubunifu na husaidia ulali wa kijinsia, mwalimu kulimudu darasa kutokana na wanafunzi kuwa bize katika kushiriki katika majadiliano ya vikundi na hata hivyo kupunguza kelele zinazotokana na wanafunzi kukosa kazi ya kufanya.* Kielelezo Na.14.2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliochanganya hoja sahihi na zisizo sahihi.


14. Ufundishaji na Ujifunzaji, Ni michakato inayo
tanyika ili kupokea na kutoa Maarifa kwa
kushirikiana ili kufikia kiwango fulani kwa
kuchunguza vitu Mbalimbali kwenye Mazingira
Ziliatazo ni faida sita za kutumia njia
ya Majadiliano ya Vikundi katika mchakato
wa Ufundishaji na Ujifunzaji.
Kupatikana kwa maarifa mbalimbali, Hii ni
faida ambayo maarifa aliyonayo mwanafunzi mmoja
dio sawa na Mwingine na Mwingine anamaarifa
yake kwaiyo ya kiunganishwa pamoja kutoa Maarifa
Kuwepo kwa Matumizi ya lugha sahihi, Hii
ni faida moja wapo kambayo wakati wa kujadiliana kuwezesha lugha sahihi kutumia ambayo
siyotofauti kuwepo kwa matumizi ya lugha.

Kuwezesha Swali Kufanyika kwa Muda mdh
ache yaani Ukombozi wa Muda, Mbinu ya maja
diliano inakomboa Muda kwa sababu Unaambi
wa jadilini kwa dakika 5 na zenyewe -
Unazitendea haki kisha kuzipatia Majibu.
Kuwepo kwa Ushirikiano baina ya Mwa
limu na Wanafunzi wake, Hakuto kuwepo na
kelele zisizokuwa na Maana bali zitakuwepo
za Kushirikiana kwa Mwalimu na Mwanafunz
Kuwepo kwa Ushirikiano baina ya Wana
funzi kwa Wanafunzi, Hii ni kweli ni faida
kwa sababu kila Mwanafunzi kwenye
kikundi anajadili na anajaribu kwa namna
anavyo fahamu yeye.
Usikilizaji wa kina wakati wa Majadili
ana Hii inawezesha na nifaida kwa
sababu baada ya kukaa kwenye kikundi
kuna mmoja atachaguliwa na kusimulia
alicho kijadili.
Hivyo basi, Mbinu ya Majadiliano
imebeba faida mbalimbali na kuweza -
kufundisha vizuri ila Unapaswa kuzifa
nya kwa kina maana panaweza kutokea
changamoto.

Kielelezo Na. 14.2: Sampuli ya majibu yenye usahihi wa wastani katika swali la 14

Katika Kielelezo Na. 14.2 mtahiniwa katika hoja sita alizotoa hoja mbili ndizo zilikuwa sahihi (hoja ya 4 na ya 5) lakini alishindwa kutoa ufafanuzi mzuri kuhusu faida za kutumia njia ya majadiliano ya vikundi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

## 2.4 SEHEMU D: UTAFITI WA KIELIMU, UPIMAJI NA TATHMINI

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (2) ya kujieleza; swali la 15 na 16. Kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15). Watahiniwa walitakiwa kujibu swali moja.

### 2.4.1 Swali la 15: Tathmini katika Elimu

Swali lilimtaka mtahiniwa atumie hoja sita kuchambua umuhimu wa tathmini katika elimu. Jumla ya watahiniwa 2,595 sawa na asilimia 88 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa, watahiniwa (99.6%) walipata alama kuanzia 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 15.




***Chati Na. 15:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 15*

Chati Na. 15 inaonesha kuwa, watahiniwa (0.4%) walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5; Watahiniwa (46.6%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa (53%) alama kuanzia 10.5 hadi 15.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa wengi 1,376 (53%) waliopata alama kuanzia 10.5 hadi 15 waliweza kuchambua umuhimu wa tathmini katika elimu. Watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Tathmini katika Elimu*. Baadhi ya majibu sahihi ya watahiniwa katika swali hili yalikuwa kama ifuatavyo: *humsaidia mwalimu kufanya maboresho ya mbinu za kufundishia na kujifunzia, tathmini humfanya mwanafunzi ajitambue, tathmini husaidia wizara ya elimu kufanya*

*maboreho katika masuala ya kielimu, tathmini humsaidia mwalimu kufanya maboresho ya zana za kufundishia na kujifunzia, tathmini humsaidia mwalimu kutambua tabia na mienendo ya wanafunzi na kuirekebisha, huwezesha serikali kuchagua wanafunzi wanaofaa kuendelea na ngazi fulani ya elimu.* Kielelezo Na. 15.1 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi.

15. Tathmini katika elimu, ni Vitendo cha kukusanya taarifa zinazohusu taaluma ili kuzichambua na kuzitafiri na kuona namna za kutatua changa moto zinazokabili ufundishaji na ujifunzaji. Tathmini huangalia Maarifa, Stadi, ujuzi na Mielenendo waliyoipata walimu na wanafunzi kama inakidhi lengo la Mtaala.

Rifuatazo ni hoja zinazoongesha/kuchambua umuhimu wa tathmini katika elimu.

Husaidia kufanya Mabadiliko ya Mtaala, baada ya kukusanya data/taarifa katika elimu njia sahihi huchukuliwa ili kuweza kufanya Maboresha ya Mtaala, kwa Mfano kuandaa Mtaala unaozingatia Matakwa ya jamii/taifa kwa Ujumla.

Husaidia kuanda vigezo katika ngazi ya elimu, kwa wanafunzi wanavendelea na ngazi za juu. Tathmini katika elimu hutumia Matokeo ya upimaji ili kuweza kuandaa vigezo vya wanafunzi kuendelea na ngazi za juu za elimu, kwa Mfano daraja lipi ni sahihi kuendelea na Mafunzo.

Husaidia kuandaa Mikakati ya kuboresha Mbinu za Ufundishaji, tathmini hutumia Matokeo ya upimaji ilikuona kama kunamadhaifu katika Mbinu za kufundishia hivyo kufanya Maboresho ya Mbinu za kufundishia kulingana na walengwa mfano njia shirikishi kama vile Matumizi ya vitendo.

Husaidia kutambua utekelezwaji wa Mtaala, tathimini hufanyawa ili kusaidia kujua Maarifa na stadi walizopata wanafunzi zinaendana na Malengo yaliyomo katika Mtaala, hivyo njia sahihi za kuweka Mikakati ya utekelezaji wa Mtaala huchukuliwa.



15 Husaidia kutatua Changamoto za Ujifunzaji na Ufundishaji, Mfano Miundombinu Mibovu katika Mazingira ya kutolea elimu, Uhaba wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, hivyo baada ya kufanya tathimini njia sahihi za kuboresha na kuzikabiri changamoto hizo hufanyika.

Husaidia kupata wataalu wazuri, tathathmini huweza kuonyesha namna yakupata wataalu kulinga na na ngazi ya elimu, kwa Mfano husaidia kufahamu aina ya walimu wanaopaswa kufundisha ngazi tofauti za elimu kama vile Shule za Msingi, na Sekondari kulinga na aina ya Mtaala huika.

Tathimini katika elimu hufanywa kwa kutumia Matokeo ya upimaji pamoja na Zana za Upimaji kama vile dodoso, ili kuweza ~~kupa~~ kubaini Changamoto Zinazoukabili Mfumo Mzima wa elimu na kufuata njia ya kukabiliana na Changamoto hizo hivyo kuweza kutoa elimu kulingana na Mabadiliko ya Sayansi na teknolojia na Matakwa ya jamii husika.

Kielelezo Na. 15.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 15

Watahiniwa 1,209 (46.6%) waliopata alama kuanzia 6 hadi 10.5 walitoa maelezo ambayo hayakujitosheleza katika kutetea hoja zao. Baadhi yao walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho vinavyojitosheleza na wengine walitoa hoja pungufu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache 10 (0.4%) waliopata alama kuanzia 0 hadi 5.5 walikuwa na maarifa kidogo kuhusu umuhimu wa tathmini katika elimu hivyo walishindwa kutoa majibu yaliyohitajika. Baadhi ya majibu yaliyotolewa na watahiniwa hawa ni: *kufanya jamii kuweza kuepukana na baadhi ya taratibu zisizoendana na wakati na kuendana na ulimwengu wa sayansi na teknolojia kupitia wanafunzi wao, husaidia kuonyesha nguvu, jitihada na juhudi za serikali hazipotei bure, kusaidia kukuza maarifa na stadi mbalimbali, kusaidia kukuza elimu na kufikia katika viwango vya juu, husaidia katika kufanya utafiti wa elimu, moja kati ya umuhimu wa kufanya tathmini ni husaidia watafiti wa elimu wanapokuwa wanafanya utafiti wa masuala ya elimu katika kuboresha sekta ya elimu jamii*

Kielelezo Na. 15.2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kuelezea hoja kulingana na matakwa ya swali.

15 Tathmini katika Elimu Niuchambuzi
unaowezo katika kufanya Uamuzi wa
jambo fulani katika elimu. Mfano
uamuzi wa kubadiliko sera ya elimu. Zifa
ataso ni hoja muhimu za kuchambua
umuhimu wa tathmini katika Elimu
ni kama ifuatavyo;
Husaidia kujua Mabadiliko ya
Kielimu hii ni kwa sababu katika
uchambuzi wa tathmini katika elimu huw
ezo kutusaidia kujua mabadiliko ya Kielimu
Husaidia kujua Mabadiliko katika elimu,
hii ni kwa sababu katika uchambuzi
wa tathmini katika elimu huwezo kujua
Mabadiliko ya Elimu.
Husaidia kujua Mabadiliko ya mtaala
katika elimu, hii ni kwa sababu katika
uchakato rasimu wa uchambuzi wa umuhimu
wa tathmini katika elimu huwezo kutu
saidia katika jinsi mtaala uliyo badili
ko wa Kielimu.
Husaidia kujua changamoto za wafanya
kazi katika elimu mfano walimu, hii
ni kwa sababu katika uchambuzi wa
tathmini katika elimu huwezo kujua changamo
to za walimu wakiwa kazini.
Husaidia kujua utekelezaji wa
sera mpya ya Elimu hii ni kwa
sababu katika uchambuzi huwezo —
kupata umuhimu wa tathmini katika
elimu. Mfano Tathmini inapokuwa ina
fanyika huwezo kujua utekelezaji wa sera ya Elimu



15. Husaidia kujua ubora wa mtaala katika elimu hii ni kwa sababu katika uchambuzi katika tathmini huwa kusaidia kujua ubora wa mtaala katika elimu jinsi unavyo fuatika.

Hivyo basi kama tulivyo ona hapo juu umuhimu wa tathmini katika Elimu jinsi unavyo weza ~~kufuatika~~ kwa na faida katika Elimu. Mfano Husaidia kujua Mabadiliko katika ~~elimu~~ mtaala pamoja na Husaidia kujua Mapungufu ya mtaala katika Elimu.

Kielelezo Na. 15.2: Sampuli ya majibu yenye mapungufu katika swali la 15

Katika Kielelezo Na. 15.2 mtahiniwa alitoa baadhi ya hoja sahihi lakini alishindwa kuelezea kuhusu umuhimu wa tathmini katika elimu na hivyo alipata alama za chini.

### 2.4.2 Swali la 16: Utafiti katika Elimu

Swali lilimtaka mtahiniwa atumie hoja sita kuthibitisha kuwa elimu bila utafiti ni kazi bure. Jumla ya watahiniwa 351 sawa na asilimia 11.9 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa 95.2% ya watahiniwa walipata alama kuanzia 6 hadi 14.5 kama inavyoonekana katika Chati Na. 16.




***Chati Na. 16**: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 16*

Chati Na. 16 inaonesha kuwa, watahiniwa (4.8%) walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5; watahiniwa (78.3%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa (16.9%) alama kuanzia 10.5 hadi 15. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulianzia alama 0 hadi 14.5.

Uchunguzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 59 (16.9%) waliopata alama kuanzia 10.5 hadi 14.5, waliweza kuthibitisha kuwa elimu bila utafiti ni kazi bure kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Utafiti katika Elimu.*Watahiniwa hawa walitoa majibu sahihi ambayo ni: *utafiti husaidia kugundua kanuni zinazosaidia kuelezea nadharia mbalimbali, utafiti husaidia kuthibiti viwango vya elimu, utafiti husaidia kujiwekea malengo ya elimu ya baadae, utafiti huwezesha mwalimu kupata ujuzi, maarifa na stadi mbalimbali.* Kielelezo Na. 16.1 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi.

16. Utafiti wa kielimu, Ni uchunguzi unaotumiambimu za kuwayunsi katika kukusanya taarifa mbalimbali zinazohusiana na masuala ya kielimu mfano utoro wa wanafunzi, na uhaba wa walimu. Hivyo elimu bira utafiti ni sawa na kazi bure kwa sababu zifuatazo:

Utafiti husaidia katika uboreshaji wa miundo mbinu ya shule, Mfano Madarasa, vyoo pamoja na nyumbam za walimu ambapo bila kufanya utafiti wa kielimu suala hili litakuwa gumu.

Husaidia katika kurekebisha mtaala, Pia kupitia taarifa mbalimbali za maendeleo ya wanafunzi katika ogyfunziaji zinazochukuliwa na watafiti huweza kusaidia katika Maboresho ya mtaala.

Husaidia katika kuongeza vyao vya kufundishia na kujifunza, Mfano vitabu ambapo bila kufanya utafiti za maendeleo ya wanafunzi aidha katika kujifunza suala kama hili huliwezi kutekeleza kwa wakati.

Humsaidia mwalimu katika kuboresha mbinu za kufundishia na kujifunzia. Mfano kwa kufanya utafiti mdogo kuhusiana na kufeli kwa wanafunzi hivyo huweza kutambua aidha chanzo ni ufundishaji hivyo husaidia katika kuboresha mbinu za kufundishia.

Huweza kusaidia katika kuajiri walimu, Pia kupitia watafiti mbalimbali wa kielimu huweza kusaidia katika ogira za walimu kutokana na changamoto ambazo walizukuta katika shule kwa kutoa taarifa katika nyazi husika.



Kielelezo Na. 16.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 16

Aidha, watahiniwa 275 (78.3%) waliopata alama kuanzia 6 hadi 10.5 walishindwa kufafanua majibu kwa usahihi na wengine walitoa hoja pungufu. Baadhi yao walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Wengine walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho vinavyojitosheleza hivyo walipata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache 17 (4.8%) waliopata alama kuanzia 0 hadi 5.5 hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya *Utafiti katika Elimu* kwa kuwa walieleza hoja zisizosahihi kulingana na matakwa ya swali. Mtahiniwa mmoja kwa mfano, alitoa hoja zifuatazo: *elimu huhitaji ushirikiano wa jamii, elimu haiwezi kufahamika bila utafiti, elimu haiwezi kubadilishwa bila utafiti, elimu inaweza kutatuliwa tatizo lake kwa kutumia utafiti, utafiti ndio jawabu la elimu*. Kielelezo Na. 16.2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



16. Elimu ni ngazi ambayo mtu andanza kusoma akiwa na umri wa miaka moja na kuendelea ili apate ~~masur~~ mafunzo mazuri ya matumizi ya baadae.

Utafiti ni hali ya kutafuta data au habari katika sekta mbalimbali ili kufamb ua kinachoendelea au kilichopo.

Elimu bila utafiti ni kazi bure ni kweli kabisa. Yafuatayo;

Elimu na utafiti unatumika kwa pamoja kwa sababu elimu haiweza kufundishika kwa ajili ya vitabu tunavyofundisha vinayanyo utafiti ~~kazi~~ vinakubalika kwenye mitaala na ufundishaji.

Kila wazazi wanaenda kufanya utafiti shule kama wanafundisha yyema na kuwapele-ka watoto wao hapo.

Kuna watafiti wanatembelea kila shule kuangalia jinsi gani wanafunzi wanafundi-shwa na kufambua changamoto zao ya hapo shuleni.

Vitabu vyote vya kiada na ziada vina-fanywa utafiti na wizara na vinakubalika kutumika na walimu na wanafunzi.

Kielelezo Na. 16.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 16

Katika Kielelezo Na. 16.2 mtahiniwa alitoa hoja pungufu na zinazohusu vitabu vinavyotumika kufundishia na kujifunzia na ufuatiliaji wa ufundishaji na ujifunzaji badala ya kueleza umuhimu wa kufanya utafiti katika elimu.

## 2.5 SEHEMU E: MISINGI YA ELIMU

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili; swali la 17 na swali la 18. Kila swali lilikuwa na alama 15 ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja.

### 2.5.1 Swali la 17: Maendeleo ya Elimu Tanzania

Swali lilimtaka mtahiniwa atumie hoja sita kutathmini elimu ya jadi kwa kufafanua sababu za msingi zilizosaidia kumfanya kila mtu aonekane ni mwalimu wa watoto katika jamii yake tofauti na sasa. Jumla ya watahiniwa 571 sawa na asilimia 19.4 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa watahiniwa 65.7% walipata alama kuanzia 6 hadi 13 kama inavyoonekana katika Chati Na. 17.




***Chati Na. 17**: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 17.*

Chati Na. 17 inaonesha kuwa, watahiniwa (34.3%) walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5; watahiniwa (55.9%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa (9.8%) alama kuanzia 10.5 hadi 15. Hata hivyo, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulianzia alama 0 hadi 13.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 56 (9.8%) waliopata alama kuanzia 10.5 hadi 13, waliweza kutathmini elimu ya jadi na kufafanua sababu za msingi zilizosaidia kumfanya kila mtu aonekane ni mwalimu wa watoto katika jamii yake tofauti na sasa kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ndogo ya *Historia ya Elimu Tanzania* hivyo walitoa majibu sahihi. Kielelezo Na. 17.1 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi.



17. Elimu ya jadi ni elimu iliyotolewa kabla ya kuja kwa wakoloni ambayo ilikuwa inahusu jando na unyago na maisha ya kila siku ya watu. Elimu hii ilimfanya kila mtu aonekane kama ni mwalimu wa mtoto katika jamii kwa haja zifuatazo.

Malengo; malengo katika elimu ya jadi yalisisitiza utumaji na uendelezaji wa mila na desturi za kiafrika, hivyo kuwafanya wanajamii kuzitishi mila na desturi hizo kwa kushirikisha jamii nzima.

17 Taratibu za utoaji masomo; masomo yaliyotolewa hayakufanga mitaala bali kila mtu mwenye uelewa alikuwa ni mwalimu wa mwenzie kwa kumfundisha - shughuli mbalimbali na namna ya kuishi.

Madhumuni ya elimu; madhumuni ya elimu ya jadi yalikuwa ni kuwezesha mtu kuishi ipasavyo katika jamii na pia kushirikiana katika utendaji baina ya wanajamii.

Ufundishaji; ufundishaji katika elimu ya jadi ulienga vitendo na hivyo kumfanya kila mtu kuwa mwalimu wa mtoto katika jamii yake tofauti na sasa.

Tathmini; tathmini ya elimu ya jadi ilifanyika kwa vitendo zaidi na kupelekea mtu yoyote mwenye uelewa na mambo hayo kumtathmini mwenzake na kuweze kumrekebisha.

Faida za elimu ya jadi; elimu ya jadi ilikuwa na faida ambazo zilipelekea wanajamii kujitegemea katika utendaji, mfano elimu ya jadi ilimuwezesha mtu kujifunza kitu anachokihitaji, ilihusisha jamii nzima na pia ilizingatia mila na desturi za waafrika, hivyo kuwafanya wanajamii kuwa walimu ambayo ni tofauti na sasa.

Hivyo mila na desturi za waafrika zilendelezwa ipasavyo ili kuwawezesha wanajamii kuendana na majukumu yao mfano utunzaji na kilimo.

Kielelezo Na. 17.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 17

Aidha, watahiniwa 319 (55.9%) walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10.5 kwa kuwa walishindwa kufafanua hoja kwa usahihi. Vilevile walitoa hoja pungufu na walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Baadhi yao pia

walishindwa kutoa maelezo yaliyojitosheleza katika sehemu ya utangulizi na hitimisho na hivyo walipata alama za wastani.

Watahiniwa 196 (34.3%) waliopata alama kuanzia 0 hadi 5.5 walikuwa na maarifa kidogo kuhusu dhana ya *Elimu ya Jadi* kwa kuwa walishindwa kutoa hoja zinazotathmini elimu ya jadi na kufafanua sababu za msingi zilizosaidia kufanya kila mtu aonekane kama ni mwalimu wa watoto katika jamii yake tofauti na sasa. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alitoa hoja kama: *haikuwa na gharama, ilitolewa bila ubaguzi wa kijinsia, ilitolewa popote iwe kijiweni, nyumbani au mkutanoni, ilikuwa mali ya jamii nzima na ilitolewa bila masharti wala vigezo*. Mtahiniwa mwingine alielezea hoja zifuatazo: *hufunzwa kwa kuiga, hujifunza kwa kuona, njia ya kuabudu, kuwepo kwa sherehe za kitamaduni, kuwepo kwa jando na unyago na kuwa mfano bora kwa watoto wao*.

Watahiniwa 4 (0.1%) waliopata alama 0 hawakuwa na maarifa yoyote kuhusu dhana ya *Historia ya elimu Tanzania*. Mfano wa hoja zilizotolewa na mtahiniwa mmojawapo aliyepata alama 0 ni: *kuweza kupambana na changamoto mbalimbali za maisha, kuweza kutambua stadi mbalimbali za maisha, kuweza kutambua namna ya kushirikiana na watu mbalimbali katika jamii, kujua namna ya kushiriki shughuli za maendeleo katika jamii, kumwezesha kukabiliana na changamoto za maisha na kuweza kuwa na ujuzi wa kufanya kazi mbalimbali*. Kielelezo Na. 17.2 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

17 Elimu ya Jadi ni elimu iliyotolewa/
waliyoipata watu Kabla ya Kuja wakolo
ni. Katika elimu ya Jadi watu walifu
ndishwa Stadi Mbali Mbali Kama vile
Uhunzi, Ususi, Ujenzi wa nyumba, utu
ngaji wa Shanga, uchongaji na upishi
Zifuatazo ni Sababu Zilizosaidia Kila Mtu
aonekane Kama ni Mwalimu wa Mtoto Kati
Ka Jamii yake tofauti na Sasa
Kutokuwepo Kwa Shule. ~~Za Kutosha~~
Kabla ya Kuja wakoloni waafrika wali
Kuwa elimu yao ya Jadi ambayo ilitolewa
Kwenye Maeneo Kama vile Kwenye mit
Mikubwa na Majumbani hivyo Kila Mtu
alikuwa akitoa elimu Kwa watoto wake
au Kumpeleka Sehemu Maalumu Kama
vile Sehemu za Jando na unyago
Kukosekana Kwa wasimamizi wa
Sekta ya elimu. Kipindi cha elimu ya
Jadi Kulikuwa hakuna usimamizi Kw
enye elimu hivyo ilikuwa Kila Mtu ana
weza Kutoa elimu Kwa watoto
Pasipo Kuwa na usimamizi Maalumu
Kuwepo Kwa umoja na ushirikiano.
Kipindi cha elimu ya Jadi Kulikuwa
na umoja na ushirikiano Kwani watu
walishi Kwa Kushirikiana hivyo iliki
wa ni rahisi Kwa Kila Mzazi Kuweza
Kutoa elimu Kwa Mtoto wa Mwenza
Ko Pasipo yeye Kukuletea Matatizo
tofauti na Kipindi cha Sasa ambapo
huwezi hata Kumuadhibu Mtoto wa Mwenzako



17 Kutokuwepo kwa wataalamu au wa
imu ambao wangeweza kutoa elimu k
ipindi cha elimu ya jadi hivyo kila
mtu ambaye alikuwa na uzuzi fula
ni aliruhusiwa au alikuwa ni mwalim
u wa mtoto wake au wamuenzake
Kutofikika kwa sehemu zilizo ku
wa zikitolewa elimu ya jadi. Baadhi ya
sehemu kulikuwa hakuna miundombinu
ambayo ingefikika na watu wakaweza
kupata elimu hivyo watu walibaki
majumbani na wazazi ndiyo walikuwa
na jukumu la kutoa elimu kwa
watoto wao
Kutokuwepo kwa mwongozo yaani
mtaala maalumu ambao watoto watapata
elimu. Katika kipindi cha elimu ya jadi
kulikuwa hakuna mwongozo maalumu
hivyo kila mtu alikuwa anauwezo
wa kufundisha chochote kile kinacho
husu jamii husika
Yote kwa yote pamoja na sababu
zilizo za msingi zilizosaidia kumfanya kila
mtu aonekane kama ni mwalimu lakini
zituatazo ni changamoto za elimu ya
jadi. Ubovu wa miundombinu uhaba
wa vitaa, mtu akita. anakufa na
usuzi wake pia jamii kutotoa ushi
rikano na kutosha kwa wataalamu

Kielelezo Na. 17.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 17

Katika kielelezo Na. 17.2, mtahiniwa alieleza sababu zilizosababisha kutokuwepo kwa mfumo rasmi wa elimu kabla ya ukoloni badala ya kufafanua sababu za msingi zilizosaidia kumfanya kila mtu aonekane kama ni mwalimu wa watoto katika jamii yake wakati wa elimu ya jadi tofauti na sasa.

### 2.5.2 Swali la 18: Elimu Jumuishi

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kina mbinu sita ambazo mwalimu anaweza kutumia katika kuwafundisha wanafunzi wenye vipaji maalumu. Jumla ya watahiniwa 2,379 sawa na asilimia 80.6 ya watahiniwa waliofanya

mtihani walijibu swali hili. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwa kuwa watahiniwa 46.1% walipata alama kuanzia 6 hadi 14.5 kama inavyoonekana katika Chati Na. 18.




***Chati Na. 18:*** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 18.*

Chati Na. 18 inaonesha kuwa, watahiniwa (53.9%) walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5; watahiniwa (42.8%) walipata alama kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa (3.3%) alama kuanzia 10.5 hadi 15. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulianzia alama 0 hadi 14.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 78 (3.3%) waliopata alama kuanzia 10.5 hadi 14.5 walikuwa na uelewa mpana kuhusu dhana ya *Elimu Jumuishi*. Watahiniwa hawa waliweza kuelezea mbinu sita ambazo mwalimu anaweza kuzitumia katika kuwafundisha wanafunzi wenye vipaji maalum. Watahiniwa hawa pia walikuwa na uwezo mkubwa katika uandishi wa insha kwa kuwa waliweza kuandika utangulizi na hitimisho vinavyojitosheleza. Kielelezo Na. 18.1 ni sampuli ya majibu ya watahiniwa waliojibu swali hili kwa usahihi.

18 Wanafunzi wenye vipaji maalum. Niwale
wanafunzi ambao uwezo wao wa kiakili da
rasani unakuwa juu kuliko wengine
walipo darasani humo
Kuna mbinu mbalimbali ambazo mwal
imu anaweza kutumia kuwafundisha wana
funzi hao kama ifuatavyo
Kuwapa kazi za kuwafikirisha zaidi
hapa mwalimu anatakiwa awape kazi am
bazo zitawafanya wafikirie zaidi na
kuwafanya wasiwe wasumbufu na kuwa
katisha wenzao kusoma ili watulie na
wenzao waendelee kujifunza.
Kuwapa kazi ya ziada tofauti na wenz
ao wengine: hapa mwalimu anatakiwa awaona
eze wanafunzi wake kazi ili kuwafanya
watulie pamoja wasisumbue wengine.



18 Kuwawha darasa na kuwapeleka da
rasa linalofuata; hii humaanisha kuwa hapa
mwalimu atawachukua hao wanafunzi na
kuwapeleka darasa linalofuata mfano kam
a walikuwa darasa la tatu atawapeleka
darasa la nne.
Kuwa nao karibu na kuwashauri; hapa
mwalimu anatakiwa kuwa naye karibu
na kumwelekeza namna ya kuishi na
wenzake wenye uwezo mdogo na kuwa
heshimu kwa kutokuwasumbua wana
pojifunza darasani.
Kuwapa kazi ya kuwafundisha wenza
o wakisimamiwa na mwalimu; hapa mw
alimu anatakiwa awe nao karibu na kuwa
pa somo la kuwafundisha wenzao na mwa
limu kuendelea kuwasimamia ili wasile
te vurugu darasani na kuwasumbua we
ngine.
Kuwafundisha kwa kuwapa mazoezi
ya kutosha, hapa mwalimu anatakiwa
awafundishe vitu ambavyo hawavifahamu
na kuwapa mazoezi mengi yatakayo wafa
nya wawe kimya kufanya kazi na wa
siwasumbue wengine.
Hivyo basi ni vizuri mwalimu kuwa
fahamu wanafunzi wake na kuweza kujua
namna ya kuishi na wale wenye vipaji
maalum ili wote wawe sawa na wale
wenye uwezo mdogo.

Kielelezo Na. 18.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 18

Watahiniwa wengi 1,019 (42.8%) waliopata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10, walitoa hoja sahihi chache na maelezo yasiyokuwa na uhusiano na swali. Wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Baadhi yao walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho vinavyojitosheleza.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,282 (53.9%) waliopata alama 0 hadi 5.5 walikuwa na uelewa mdogo kuhusu dhana ya *Elimu Jumuishi* hivyo waliandika angalau utangulizi na hoja chache ambazo walishindwa kuzitetea. Mtahiniwa mmoja aliandika hoja kama; *majadiliano ya vikundi, kisa mafunzo, maswali dodoso, bungua bongo, changanya kete na igizo dhima.* Mtahiniwa mwingine alitoa majibu kama vile: *mbinu ya mhadhara, onesho mbinu, maswali na majibu, igizo dhima, kualika mgeni, na jozisha fikirisha andika.* Aidha mtahiniwa mwingine alielezea hoja kama vile: *ishara, vitu halisi, majadiliano, matembezi ya ghalari, maswali na majibu* na *mbinu ya nyimbo* badala ya kuelezea mbinu ambazo mwalimu anaweza kutumia katika kuwafundisha wanafunzi wenye vipaji maalum. Kielelezo Na.18.2 kinaonesha majibu ya mmoja wa watahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



18 alumu kwa kuwapeleka wanafunzi kati
ka ziara inayohusu jambo fulani. mfano
kama dhana ni mabadiliko ya hali ya
hewa basi mwalimu huweza kuandaa ziar
a ya kwenda kwenye hitua cha kureko
dia vipengele vinavyounda hali ya hewa
akiwe na wanafunzi wake ambapo watafi
funza mambo mbalimbali.
Mduara ndani mduara nje. pia
mwalimu anaweza kutumia mbinu ya mduara
ndani mduara nje katika kuwafundisha
wanafunzi wenye vipaji maalumu. katika mbi
nu hii mwalimu atawagawa wanafunzi
katika maduara mawili limoja ndani ya
duara lingine kisha kuwaambia wa ndani
wawageukie wa nje na waanze kufanya ma
jadiliano kisha kuwaambia wasogee na kuwa
ambia wenzao kuhusu walichajadili.
Igizo dhima. katika mbin
u hii ~~wa~~ mwalimu ~~ataan~~ pamoja
na wanafunzi wataandaa igizo lenye
kutoa ufafanuzi kuhusu jambo fulani
mfano wanaweza kuandaa igizo lenye kio
neshe madhara ya madawa ya kulevya
na wanafunzi wakaelewa somo vizuri hi
vyo mbinu hii inaweza kutumika kufundi
sha wanafunzi wenye vipaji maalumu
Hivyo mwalimu anaweza
kutumia mbinu mbalimbali katika kuwa
fundisha wanafunzi wenye vipaji maa
lumu kwani kwa ni wepesi kuele
wa na hivyo mbinu nyingi zinaweza kutu
miwa.

Kielelezo Na. 18.2: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 18

Katika kielelezo Na. 18.2 mtahiniwa alieleza mbinu ambazo zinaweza kutumika kufundishia wanafunzi wote hata wale wasio na vipaji maalum badala ya kueleza mbinu ambazo ni mahususi katika kuwafundisha wanafunzi wenye uelewa wa juu na wenye vipaji maalumu, hivyo kupata alama pungufu.

## UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Kiwango cha ufaulu katika mada zilizotahiniwa mwaka 2021 kilikuwa kizuri kwani asilimia 99.9 ya watahiniwa walipata wastani wa alama kuanzia asilimia 40 na zaidi.

Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika mada za mtihani wa somo la Ualimu kinaonesha kuwa kati ya mada zote kumi na tatu (13) zilizotahiniwa watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri katika mada kumi (10) ambazo ni: *Makuzi na ukuaji wa mtoto* (96.9%), *Saikolojia* (87.53%), *Mtaala* (83%), *Upimaji katika Elimu* (99.1%), *Tathmini katika Elimu* (96.8%), *Uongozi wa Elimu Tanzania* (92.3%), *Ufundishaji* (80.8%), *Matayarisho ya Ufundishaji (94.8%), Elimu ya Watu Wazima* (95.4%) *na Utafiti katika Elimu* (95%). Aidha, mada tatu (3) zilikuwa na ufaulu wa wastani ambazo ni: *Nadharia za Kujifunza* (67%), *Maendeleo ya Elimu Tanzania* (65.7%) na *Elimu Jumuishi* (46.1%).

Ufaulu mzuri kwenye somo hili umesababishwa na watahiniwa wengi kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu mada zote zilizotahiniwa katika mtihani wa mwaka 2021. Uchambuzi zaidi wa ufaulu unaonesha kuwa mada tatu (3) za *Ufundishaji, Matayarisho ya Ufundishaji* na *Elimu ya Watu Wazima* zilikuwa na ufaulu mzuri kwa miaka mitatu mfululizo yaani 2019, 2020 na 2021. Kwa mfano, mada ya Matayarisho ya Ufundishaji ilikuwa na ufaulu wa asilimia 99.79, 99.1 na 99.1 mtawalia. Mada ya Ufundishaji ilikuwa na ufaulu wa asilimia 99.76, 77.9 na 80.8 mtawalia. Kwa upande mwingine, mada ya Elimu ya Watu Wazima ilikuwa na ufaulu wa asilimia 94.39, 85.6 na 95.4 mtawalia.

Kwa ujumla ufaulu katika mada za somo la Ualimu umekuwa mzuri kwa miaka miwili (2) mfululizo yaani mwaka 2020 na 2021. Hakuna mada iliyokuwa na ufaulu hafifu katika mtihani wa mwaka 2021. Ufaulu huu unaashiria kuwa ufundishaji na ujifunzaji katika vyuo vya ualimu unafanyika vizuri.

## 3.0 HITIMISHO

Ufaulu wa watahiniwa katika Mtihani wa somo la Ualimu 2021 ni mzuri kwa kuwa kiwango cha wastani cha ufaulu kwa mada zote kumi na tatu (13) kilikuwa asilimia 84.6. Watahiniwa wengi walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika dhana mbalimbali zilizoulizwa, uwezo wa kubaini matakwa ya swali na maarifa ya kutosha juu ya uandishi sahihi wa insha. Hata hivyo watahiniwa wachache walishindwa kupata alama za juu kwa sababu ya uwezo mdogo wa uandishi na ufafanuzi wa hoja hasa katika maswali ya insha na kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana mbalimbali zilizoulizwa.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa utawasaidia wakufunzi na wanachuo kuelewa dosari zilizosababisha watahiniwa wachache kutojibu vizuri maswali ili kuweza kufanya maboressho kulingana na mapendekezo yaliyotolewa kwa ajili ya kuinua zaidi ufaulu katika somo hili.

## 4.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua zaidi ufaulu kwa wanachuo katika somo hili inapendekezwa kuwa:

(a) Wakufunzi wa somo la Ualimu wawapange walimu tarajali katika vikundi vya kujisomea vyenye mchanganyiko wa wanachuo wenye uwezo wa juu na wale wenye uwezo mdogo/wastani. Mchanganyiko huu utasaidia kuinua kiwango cha ufaulu kwa wale wenye uwezo mdogo au wastani.

(b) Walimu tarajali waongozwe katika majadiliano katika vikundi na katika kuwasilisha na kusoma matini kuhusu dhana mbalimbali zilizopo katika muhtasari wa somo la Ualimu wa mwaka 2009 ili kuwajengea uwezo zaidi walimu tarajali juu ya mada za Nadharia za Kujifunza, Maendeleo ya Elimu Tanzania na Elimu Jumuishi zilizokuwa na ufaulu wa wastani.

(c) Walimu tarajali wapewe mazoezi ya kutosha kwenye dhana mbalimbali za somo la Ualimu na kutakiwa kuwasilisha mara kwa mara insha ya mtu mmoja mmoja ili kuwajengea uwezo katika uandishi sahihi wa insha.

(d) Wakufunzi watumie mbinu ya ziara kwenye shule zilizo na wanafunzi wenye mahitaji maalum hasa wale wenye vipaji maalumu ili kuwajengea uwezo zaidi juu ya mada ya *Elimu Jumuishi*.

**Kiambatisho**

## UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA ZA SOMO LA UALIMU

| Na. | Mada | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ufaulu katika kila swali (%) | Wastani wa ufaulu katika kila swali (%) | |
| 1. | Upimaji katika Elimu | 8 | 99.1 | 99.1 | Vizuri |
| 2. | Makuzi na ukuaji wa mtoto | 12 | 96.9 | 96.9 | Vizuri |
| 3. | Tathmini katika Elimu | 3 | 94 | 96.8 | Vizuri |
| | | 15 | 99.6 | | |
| 4. | Elimu ya Watu wazima | 6 | 95.4 | 95.4 | Vizuri |
| 5. | Utafiti katika Elimu | 16 | 95.1 | 95.1 | Vizuri |
| 6. | Matayarisho ya ufundishaji | 10 | 94.8 | 94.8 | Vizuri |
| 7. | Uongozi wa Elimu Tanzania | 9 | 92.3 | 92.3 | Vizuri |
| 8. | Saikolojia | 1 | 98.5 | 87.5 | Vizuri |
| | | 11 | 93.0 | | |
| | | 5 | 71 | | |
| 9. | Mtaala | 2 | 83 | 83 | Vizuri |
| 10. | Ufundishaji | 7 | 51.2 | 80.8 | Vizuri |
| | | 14 | 99.7 | | |
| | | 13 | 91.6 | | |
| 11. | Nadharia za Kujifunza | 4 | 67 | 67 | Wastani |
| 12. | Maendeleo ya Elimu Tanzania | 17 | 65.7 | 65.7 | Wastani |
| 13. | Elimu Jumuishi | 18 | 46.1 | 46.1 | Wastani |